# MSIOGOPE

Na tuendelee kusimama kwa muda mfupi tu tunapoinamisha vichwa vyetu mbele za Mungu. Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa, sijui kama kuna haja maalum humu jengoni usiku wa leo, ambayo mngehitaji maombi kwa ajili yake. Acha tu ijulikane kwa mkono wako ulioinuliwa. Bwana awabariki.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia kile Kiti kikuu cha Enzi sasa, katika Jina la Bwana Yesu, kwa kuwa tunaambiwa kwamba kama tukija na kuomba lolote katika Jina Lake, tutapewa. Nasi tunataka kwanza kukushukuru Wewe kwa ajili ya kusanyiko hili zuri sana, siku hizi nne usiku za watu waliojazwa na Roho waliokusanyika pamoja hapa. Nasi tuliona ya kwamba Maandiko tena yanathibitika kuwa ni kweli, ya kwamba, "Popote wawili au zaidi wanapokusanyika pamoja, nitakuwa miongoni mwao." Nasi tumekuona Wewe ukiwaponya wagonjwa, ukitamka baraka, ukiwaambia watu yatakayotukia, nasi tunashukuru sana kwa ajili ya hilo.

3 Nasi, kama ndugu hapa jukwaani, Bwana, ninashukuru kwa ajili ya kundi hili la wanaume ambao ninajua kwamba . . . Hawa Wakristo, hawa watoto waliozaliwa upya, ambao ndio kwanza waingie ndani ya Kristo juma hili, Bwana, naomba kwamba kila mmoja wao atapata makazi ya starehe hapa, kanisa la nyumbani, na kukuishia Wewe, na kufanya kazi mpaka Yesu atakapokuja.

4 Pia jalia matokeo haya, ya sisi kukusanyika pamoja, yasababishe kuja kwa uamsho wa mtindo wa kale kote kwenye mji mzima, Bwana. Wengi . . . Jalia usiishe kamwe, mpaka Yesu atakapokuja. Jalia uamsho uweko daima. Jalia makanisa haya yajazwe, kila mahali, na Injili tukufu ya Yesu Kristo ijulikane kote nchini.

5 Sasa, Baba, tu—tunawaombea hawa wanaoinua mikono yao. Unajua kile kilichokuwa chini ya mkono huo. Sisi . . . Unajua yote kulihusu, kwa hiyo tunalikabidhi tu Kwako, na kuomba kwamba Wewe utawajalia haja yao.

6 Basi sasa tumegee mkate wa uzima, Bwana. Tunakutaka Wewe useme nasi kupitia Neno, kwa kuwa, "Imani chanzo chake ni kulisikia Neno." Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utayafanya yajulikane kwetu usiku wa leo, mapenzi Yako ya Kiungu. Jionyeshe Mwenyewe tena usiku wa leo miongoni mwetu, Baba. Tunakushukuru Wewe kwa yote ambayo yamefanywa na kusemwa, na kuutazamia huu, kuwa wakati mkuu wa upeo wa ibada hii. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

7 Ninahesabu haya kuwa moja ya majaliwa yangu makuu, kwamba tumekuwa na wakati huu wa ushirika hapa pamoja nanyi watu wazuri, hapa katika jumba hili la mikutano huku Tucson. Nami nilikuwa hapa kwa siku chache tu, na ni—nimekuwa hapa kwa siku chache, hasa, nami niliwaza labda juu ya kuja hapa na sio. . .Kuondoka bila kusema lolote, ama kufanya mkutano, kwa namna fulani lingeonekana ni baya. Na sikupata nafasi ya kuwatembelea ndugu hawa wazuri wote, ambao nimekutana nao hapa tangu nimekuwa jukwaani. Na laiti ningeweza kukaa juma moja kwenye kila kanisa. Hakika ningetaka kufanya hivyo.

8 Na, lakini, nina furaha sana ya kwamba ninyi watoto wachanga mliozaliwa upya, ninyi ambao ndio kwanza mpate Kristo juma hili. . .Kama ningalikuwa mahali penu, ni—ningejitafutia kanisa zuri la nyumbani miongoni mwa wanaume hawa hapa, popote nilipokuwa karibu napo, ama kuchagua kuhudhuria. Nayo makanisa ambayo nilitembelea, kuna baadhi ya wanaume hawa hapa, nimekuwa katika makanisa yao, watu wanaowaka moto kweli kwa ajili ya Mungu, ari inayowaka moto, wakijaribu wawezavyo kuishikilia Nuru ya Injili. Ni—ninawathamini watu kama hao. Basi, kumbukeni, watu hawa wanaamini Injili ile ile ninayosimama hapa nikihubiri. Ndio wadhamini wangu. Ndio ambao husimama hapa jukwaani. Hawaionei Hii aibu. Wanaitetea. Wanaiamini. Nao wapo hapa, wakiniunga mkono, wakiniombea, kila usiku. Nami nafikiri, kama huendi kanisani, kwa nini usiende kwenye moja ya hawa watu wazuri hapa, na—na uje katika kanisa lao na ushiriki pamoja nao. Kama ningalikuwa ninaishi hapa, na si mhudumu mimi mwenyewe, hivyo—hivyo ndivyo ningefanya. Hakika ningejitafutia kanisa zuri la nyumbani pamoja na baadhi ya watu hawa, na—na kupachukua mahali pangu katika Kristo.

9 Na ikiwa hujawahi kubatizwa bado, wewe uliyetoa moyo wako kwa Kristo, shauriana na mmoja wa watu hawa, nawe utapokea ubatizo wa Kikristo. Halafu basi, na ikiwa hujampokea Roho Mtakatifu, wa—watajua jinsi ya kukushauri, jinsi ambavyo huna budi kumpokea.

10 Nitazungumzia hilo asubuhi kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, Bwana akipenda, juu ya, kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kidogo nimejieupusha na machache ya Fundisho hapa, kwa sababu sisi ni kundi lililochanganyikana hapa ndani. Lakini, asubuhi, ninataka kuzungumza Ujumbe wa kiinjilisti kuhusu Roho Mtakatifu, Bwana akipenda. Sasa, nafikiri kiamshakinywa kinaanza saa tatu. Saa mbili, sivyo? Saa mbili, asubuhi.

11 Na sasa ningetaka kumtaja mtu fulani ambaye tumejaribu, tangu tumekuwa hapa Tucson, kumpata. Na labda, baadhi yenu ndugu hapa, huyo mama huenda ni mfuasi wa kanisa lako. Nafikiri anaitwa kwa jina la Charlotte Raney. Je, mtu yeyote. . .

Mnamjua? Yeye yupo hapa jijini? Charlotte, upo hapa? Mimi—mimi... Yeye ni rafiki yetu binafsi, nasi tusingeweza kumpata. Yeye ni nesi.

12 [Mtu fulani anasema, "Binti yake yupo hapa."—Mh.] Binti yake. Vema, jamani, jamani! Sijui yeye ni mkubwa vipi? Simama, kipenzi, popote ulipo. Natumaini wewe si mkubwa kupita kiwango hata ningekuita kipenzi. ["Yule pale."] Loo, loo, jamani! Karibu umepita ukubwa huo wa "kipenzi," sivyo? Asante. Mwambie mama, "Mungu ambariki; na tunampenda; na hakika tungependa kumwona kabla hatujaondoka." Na basi mpate tu yeyote wa...Billy Paul ama yeyote hapa, na hebu tujue unakoishi. Tumejaribu kukupata kwa kitabu cha orodha ya simu. Tumeuliza-uliza huku, kila mahali, na tusingekupata. Asante, sana. Na wakati wa mwisho nilipokuona, ulikuwa ni kitoto kidogo tu.

Huyu Bibi Raney, dada ya—ya—yake.

13 Nesi mwenye sifa sana, alikuwa ni mmoja wa wagonjwa wa kwanza wa kansa niliomwona Bwana akiponya. Hata hakujua mahali alipokuwa, wala chochote kile, amechomwa na radiamu. Naye Bwana alikuwa tu ndiyo kwanza aniite kwenye huduma hii, siku moja ama mbili usiku hapo kabla. Loo, ni miaka mingi, mingi iliyopita, labda miaka ishirini, miaka ishirini na mitano iliyopita. Naye alikuwa Louisville, na kwenye kumbukumbu ya kansa, huko Louisville, amekuwa amekufa, miaka ishirini. Naye anafanya kazi ya nesi sasa, na mwenye afya na nguvu tu awezavyo kuwa.

14 Na huyu ni dada yake aliyekuja Magharibi hapa, na yeye na yule mtoto mchanga, ilikuwa ni wakati huo. Na tangu tumekuwa hapa, tumekuwa tukijaribu kuwapata. Basi nilimwambia Meda ya kwamba ningeninii...mke wangu...nilikuwa nimeangalia kila mahali, na ni—nisingeweza kumtambua. Ndipo nikafikiri labda kwamba—kwamba alikuwa amehama, ama kitu fulani. Nami, kila usiku, nilifikiri nitampigia simu. Ndipo nikaandika, mambo fulani hapa chini, niliyotaka kusema, kwenye karatasi fulani, nisije nikasahau. Ninazeeka.

15 Nilikuwa nikimwambia Ndugu Moore. Ni wangapi wanaomfahamu Jack Moore? Hakika, mnamfahamu, nyinyi Wafanyabiashara Wakristo. Mhudumu mzuri huko Shreveport. Alikuwa ni mmoja wa wenzangu katika mkutano. Nikasema, "Ndugu Jack, unajua, inakuwa ni vigumu kwangu kukumbuka tena kama nilivyokuwa nikifanya. Ilikuwa kwamba, ningeweza tu kukumbuka chochote, upesi sana."

"Loo," anasema, "huo ndio umbali wote ulioenda?"

Nikasema, "Huo ni umbali wa kutosha."

16 Akasema, "Jamani!" Kasema, "Mimi humwita mtu, kwenye simu, kasema, 'Unataka nini?'"

17 Hiyo ni—hiyo ni mbali sana barabarani. Yeye ni mkubwa kuliko mimi kwa miaka minne au mitano. Natumaini sitafikia hapo. Alikuwa tu akisema hilo, hata hivyo. Yeye ni Mwairishi, ucheshi. Lakini, kumpigia mtu simu na kumwuliza alitaka nini, hilo lingekuwa ni baya.

18 Sasa, jambo lingine, ninakushukuru, dada, kipenzi, na uhakikishe u—umetupata. Mwambie mama tunataka kumwona, nasi tunarudi kumwona Shangazi Margie, mara moja, Mjomba Bill.

19 Sasa, ninashukuru, ninashukuru sana, kundi hili la wahudumu ambao walidhamini programu hii hapa. Na kwa Wakristo . . . Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel hapa wa mjini, ninashukuru.

20 Mimi hujaribu kuingia kila mahali padogo ninapoweza, nasi hatuwezi kwenda kwa yote. Huyu hapa meneja wangu, ameketi papa hapa, Ndugu Borders, ambaye huambatana nami na kuitayarisha mikutano. Nami nina kitabu, nyumbani, karibu kama *hivyo*, kilichojaa mialiko, kote ulimwenguni, na wananiambia ana kingine anachopaswa kunipa asubuhi.

21 Lakini kwa kawaida mimi huenda tu kule Mungu anakoniongoza. Basi, ninapoenda kule, ndipo ninaweza kuja katika Jina la Bwana Yesu, kwa sababu Yeye alinituma kama balozi. Nami nilijisikia kuongozwa, wakati nilipokuwa hapa Tucson, kufanya mkutano huu. Nilifikiri ingekuwa ni vema, na hasa sana kupata kufanya ushirika.

22 Na ni wangapi wanaomkumbuka Fred Bosworth, Ndugu F. F. Bosworth, yule mzee mtakatifu mashuhuri wa Mungu? Na yeye ndio kwanza aende nyumbani Utukufuni, kwenye umri wa miaka themanini na minne, hivi majuzi tu. Naye alisema, “Ndugu Branham, unajua ushirika ni nini?”

Nikasema, “Ninafikiri ninajua, Ndugu Bosworth.”

23 Akasema, “Ni jamaa wawili katika chombo kimoja tu.” Kwa hiyo, ninayo nafasi kwa ajili ya huyo mwingine, kwa hiyo ninashukuru sana.

24 Na hiyo daima hunikumbusha juu ya hadithi ndogo. Nilikuwa nikiingia, huko nje, mmoja wa mabawabu akakutana nami na kunipa mkono. Akasema, “Aisee, mhubiri,” kasema, “Mimi—mimi ni ndugu mwenzako.”

25 Nikasema, “Nina furaha kukutana nawe.” Na akaniambia jina lake, naye alikuwa ni Muairishi, pia.

26 Na kwa hiyo mtu fulani aliniuliza, wakati mmoja, kasema, “Wewe ni wa taifa lipi, Ndugu Branham?”

27 Nikasema, “Mimi ni Muairishi.” Na kama kuna . . . Na kama wanaweza kuokolewa, kuna tumaini kwa ajili ya ulimwengu mzima.

28 Na kwa hiyo—na kwa hiyo ilitokea kwamba yeye ni Muarishi, pia. Basi akasema, "Ninapenda hizo hadithi kuhusu kuwinda." Akasema, "Ninapenda kuwinda, pia."

29 Kwa hiyo, vema, "Inakubidi kuwa mambo yote, kwa watu wote," mwajua, "tupate kuwaleta wengine kwa Kristo."

30 Basi tukizungumza juu ya ushirika, ninakumbuka wakati mmoja, nami nilikuwa huko New Hampshire ya kaskazini. Nilikuwa...Huko ndiko makazi ya kulungu wenye mikia myeupe. Nilikuwa nikivua samaki kwa ajili ya hawa samaki wa hudhurungi na wenye mikia miraba. Nasi...nami nilikuwa na mahali, pamejaa kabisa, maskini hema langu lilikuwa huko juu kabisa, mlimani. Loo, niliona mahali ambapo maji yalikuwa yakitiririka juu ya ninii...

31 Nami ninajua nina marafiki wengi wavuvi. Sijapata maji ya kutosha katika Arizona kwenda kuvua samaki, bado, tangu nimekuwa hapa. Ninayanywa yangu yote. Lakini ni ninii tu... Hilo ndilo jambo pekee. Mimi, ninaipenda nchi hii, lakini laiti tungalikuwa na maziwa ama vidimbwi, ama kitu fulani huku. Nami ni Mbaptisti, mwajua, na kwa namna fulani ninapenda maji mengi. Na kwa hiyo wao...

32 Nilikuwa na kidimbwi hiki ki—kidogo nilichokuwa nikivulia. Loo, jamani! Ninawashika tu, mwajua, kama tu kucheza nao, kisha ninawaachilia. Na kama nikimwua mmoja, hakika, ningemla huyo. Na huku nyuma ya ugwe wangu, nimekuwa nikishika kundi la samaki wadogo wa majini kule nyuma.

33 Kwa hiyo nililala usiku kucha kwenye hema dogo, nilikuwa kule siku kadhaa. Ndipo kesho yake asubuhi, nikachukua shoka langu dogo la mkono, nikaondoka. Nilifikiria ningefyeka vichaka hivyo, na kucheza kidogo na hao samaki wa maji baridi. Wakati mwingine, yapata kesho, nitashuka niende tena, hema langu dogo mgongoni mwangu.

34 Basi nikiwa njiani nikirudi, kulikuwako na ma—mama dubu na watoto wake wawili waliokuwa wameingia kwenye maskini hema langu dogo la gunia. Kwa hiyo, na si kile walacho, ni kile wanachoangamiza. Loo, jamani! Wanapenda kuchacharisha vitu. Wao ni Wapentekoste, kamili, hivyo. Kwa hiyo wa—wananinii tu—wanapenda tu...Wanapenda tu hilo. Kwa hiyo wanaingia na kuangusha bomba la moshi wa stovu, na kuliponda-ponda kabisa. Sasa, tukizungumza kuhusu kelele, vema, afadhali niliache hilo. Mnaona?

35 Ninaweza kuthibitisha, chochote kisicho na mhemuko ndani yake kimekufa. Kwa hiyo iwapo dini yako haina mhemuko kidogo ndani yake, afadhali uizike, kisha—kisha upate kitu fulani. Inakubidi kuwa na mhemuko ili kuwa hai.

36 Basi kwa hiyo angalia, maskini ninii hii...Nilipokuja, nilisikia kelele. Ndipo nikaangalia kule, na hapo alikuwako

maskini mama dubu na jamaa wake wawili wadogo, walikuwa wameingia mle. Nao walivuruga tu kila kitu kilichokuwako. Kwa hiyo nilijua hiyo ilikuwa ni “kuivuruga kambi kabisa kisha kuondoka.” Kwa hiyo basi nikaangalia, na maskini huyo mama dubu, akakimbilia upande mmoja. Kisha akaita, mwajua. Alikuwa ni dubu mweusi. Hao si wakubwa sana. Na kwa hiyo akakimbia na kumwita mtoto wake. Ndipo mmoja wa hao watoto akamjia, na huyo mwingine hakuja. Vema, nikashangaa, “Kwani kuna nini?”

37 Nami nilikuwa na bastola ya kale iliyochakaa imewekwa mle kwenye hilo hema. Na, ila, nadhani ilikuwa imevunjiliwa mbali kufikia wakati huo. Nami nilikuwa nimelishika lile shoka mkononi mwangu, na—nami . . . Mwajua, maskini mama dubu mwenye watoto, anaweza kwa namna fulani kukasirika, mwajua. Naye anaweza kukukwaruza, pia, alitaka kufanya hivyo. Kwa hiyo kwa namna fulani nilikuwa nikimwangalia, mwajua, nikiweka mti niani wakati wote. Kwamba ningeweza . . .

38 Mmesikia habari za yule mhubiri kwenye mti wa perisomoni, vema, aina yoyote ya mti itafaa kama dubu anakufukuza. Kwa hiyo nikauangalia huo mti, nami nikashangaa maskini dubu huyo mdogo alikuwa na shida gani. Alikuwa ninii tu . . . hakuwa anaondoka. Naye mama yake akaendelea kumwita, naye akaendelea tu kuketi. Amejikunyata kabisa, namna *hii*. Nikawaza, “Kwani maskini jamaa huyo amepata nini?” Nikawazia labda ningeweza kuingia ndani upesi na kuinyakua maskini ile bastola. Nikawaza, “Loo, nisingemwua maskini huyo mama dubu, kama angenishambulia, kwa sababu angewaacha mayatima wawili msituni. Kwa hiyo nisingefanya hivyo.

39 Kwa hiyo nikawaza, “Nitauangalia tu mti huu, na nione jamaa huyo mdogo ana nini.” Na sasa alikuwa amejikunyata kabisa, namna *hii*, nami nikamwona akisogea. Naye maskini yule mama alikuwa akiita, na akienda huku na huku, kwa namna fulani hana utulivu. Naye alikuwa akiniangalia, pia. Ndipo alipougeuza mgongo wake kumwangalia huyo dubu mwingine, nilikuwa nimejongea kando, namna *hiyo*, kujaribu kukaribia, nione ni kitu gani jamaa huyo mdogo alikuwa . . . kilichomvutia sana. Mnajua alichokuwa nacho? Alikuwa na ndoo yangu ya sukari ya rojorojo.

40 Nanyi mwajua, na—napenda chapati maji. Ninajua nina wananchi wenzangu wenye hamu hiyo hiyo ya chakula. Kwa hiyo, na—nami najua si—siamini katika kunyunyizia. Ninapenda kuzibatiza kwelikweli. Ninapenda kuzimwagilia kabisa, mwajua, kutia sukari nyingi ya rojorojo. Mara ya mwisho nilipokula hapa chini kwenye Ramada, hivi majuzi, tulikuwa na kiamshakinywa kizuri sana. Nao walikuwa na magole mazuri, namna hiyo. Tunayaita magole, huko Kusini. Lakini ninyi . . . Kama tukiyala asubuhi, mwambie mhudumu sukari ya

rojorojo kidogo tu zaidi, tafadhali. Hiyo, hiyo haikutosha. Kitu hicho, nilichokuwa nacho, nikaweka sukari juu yake, mwajua, kumalizia.

41 Lakini, hata hivyo, maskini dubu huyu mdogo, jamaa huyo mdogo alikuwa ameninii wayo wake, na kuifungua ndoo hii. Alikuwa na ninii yake . . . Wanapenda vitu vitamu, mwajua. Naye alikuwa ameingiza maskini wayo wake ndani ya ndoo hii ya sukari ya rojorojo. Hakujua jinsi ya kuila kwa mikono yake, kwa hiyo a—anapaka tu hiyo kisha anaramba, mwajua. Kisha angepaka na kuramba, akiisha kuchovya na kumaliza ndoo yote.

42 Nikasema, "Toka hapo." Nikaendelea kumpigia makelele. Hata asingegeuka. Basi baada ya kuchovya na kumaliza ndoo kabisa, aligeuka, akaniangalia. Na asingeweza kuyafungua macho yake, mwajua. Kuanzia juu ya masikio yake, hata chini kwenye kijitumbo chake, alijaa tu sukari ya rojorojo kabisa.

43 Nikawaza, "Hiyo ni kweli. Hakuna hukumu ya dhambi. Hiyo ni kama tu mkutano mzuri wa kale wa kipentekoste. Wakati unapouingiza mkono wako moja kwa moja ndani ya ndoo ya sukari ya rojorojo, ama kopo la asali, kufikia viwiko vyako, na unapaza tu sauti, ukimsifu Mungu, sijali ni kitu gani kinaendelea, hukisikii. Unaona?

44 Lakini, unajua, jambo la kushangaza lilikuwa, alipomaliza, na hao wengine wamesimama pale nje wakimgombanisha; wakati alipofika kule, hao wengine walikuwa na ushirika. Wote walimramba. Maumbile yanashikilia mambo fulani ya ajabu, sivyo, ndugu? Kuramba yote. Sasa, hao watu ambao hawakuhudhuria mkutano huu, wanaweza tu kuramba sukari yenu ya rojorojo, kwenye . . . unaona, baada yake kumalizika. Vema.

45 Tunashukuru, tunashukuru kwa ajili ya kundi hili zuri la ndugu, na kwa hili kundi zuri la watu. Na wao . . . Nafikiri kwamba kila kitu kilitokea vema. Na sisi hatuninii . . . Sisi kwa kweli . . . Kitu kimoja ambacho hatutaruhusu ni fedha, mvuto wowote wa fedha. Ndugu aliniambia pale nje, kasema walikuwa na zote ila dola mia moja. Nikampa hundi. Nikasema, "Sahau hiyo. Mnaona? Nitailipia, mimi mwenyewe." Kwa hiyo basi—basi sisi . . . Kila kitu ni sawa na barabara. Nasi tunataka . . .

46 Kama yeyote wa wafanya kazi wa Hoteli hii ya Ramada yupo hapa usiku wa leo, ninataka kuwashukuru, kwa kuwa walitupa jengo hili bure. Ninafikiri . . . Na mimi sikuwa . . . Ninajua . . . Jinsi tu nilivyojua, ni Ndugu Tony aliyeniambia kulihusu. Ninaamini ya kwamba ni . . . kwamba kama mtu fulani alikuwa katika jiji hili, ama akitafuta moteli, bila shaka ningetangaza na kuwaambia Ramada ndipo mahali pa kwenda.

47 Kama watu wanawazia sana hivyo . . . kutuhusu sisi, na dini yetu, na Kristo wetu, nafikiri inatupasa kuwa na ujasiri wa kutosha kusema jambo zuri kuwahusu, na kumwambia kila mtu

tuwezaye. Hiyo ni kweli. Bwana na abariki taasisi hii. Daima tumeenda mahali pao popote tuendapo kote nchini. Daima tumekuwa na fadhila namna hiyo. Na Wafanyabiashara hutumia kumbi zao, Phoenix na popote tuwezapo, kufanyia mikutano na mikutano mikubwa. Nami nasema hivi, mabwana, kama mpo hapa, Mwenyenzi Mungu awabariki sana. Na kwenye mwisho wa safari, ninaomba ya kwamba Mungu ataifungua milango Yake, na kuwakaribisha kwenye Ufalme Wake mkuu wakati huo.

48 Halafu basi kuna jambo moja zaidi. Nina lundo la vitu vyenye muhtasari ulioandikwa hapa, na mafungu fulani ninayotaka kutumia katika dakika chache. Lakini, jambo jingine, ni kwamba ninyi watu mmebarikiwa sana hapa Tucson. Sasa, daima waliniambia ya kwamba Tucson ilikuwa ndipo mahali palipo karibu sana na kuzimu palipokuwapo, kwa kuwa ni joto sana. Lakini, ninawaambieni, kweli ninafurahia hii. Mbona, nyumbani kwangu kama kungekuwa na joto hivi, mbona, u—usingeweza kusimama hapa umevaa koti, kiyoyozi kikifanya kazi. Ingekuwa. . . Ungekuwa tu unatokwa jasho. Vema, kamwe sijawahi. . . Nimefanya kazi kwa bidii sana, na kamwe sijapata kutoa jasho bado.

49 Vema, ninapenda hii. Kwa nini urudi Mashariki, kwenye—kwenye msimu wa kiangazi? Hapa ndipo mahali pa kuja. Hii ni sawa. Ni bora zaidi kuliko kinamasi chetu kule nyuma, hata hivyo. Kwa hiyo, naipenda hii. Basi natumaini Bwana mwema ataniruhusu kurudi, nitoke hapa nje mahali fulani na kukaa. Na kwa kweli ninapapenda mahali hapa.

50 Na moja ya mambo makuu, matukio, moja ya sifa muhimu sana ya mahali hapa, hakika, ni watu, kile kinachopafanya mahali hapa. Mimi. . . Hata katika maduka yenu, kila kitu, na mji wa watalii, nimekuwa na baadhi ya makaribisho mazuri sana, watu wazuri kuliko wote, tangu nimekuwa Tucson, ambao hakika ningetaka kukutana nao.

51 Halafu basi nilipoingia, nilifungua redio yangu, na nikapata kituo hapa ambacho daima hakitangazi kitu ila muziki wa Kikristo. Ni kituo cha KAIR. Nami ndio kwanza nijue leo, ya kwamba makao yao makuu yako hapa kwenye Ramada. Mnajua kile nilichofanya; kama baadhi ya wafanyakazi wa KAIR wapo hapa. Nilinunua redio ili kuiweka tu imefungulia wakati wote, kusudi watoto wangu na nyumba yangu waweze kusikia kitu kifaacho.

52 Kwa kuwa, karibu stesheni zote unazofungua, daima ni namna fulani ya hii hapa bugibugi, ama chochote upuuzi huo ulicho, na—na roki, na namna hii nyingine yote ya upuuzi walio nao siku hizi. Na—na husikii kitu hicho. Nami nafikiri kwamba ninyi Wakristo, mnapaswa kufanya kila kitu mwezacho kukidumisha kituo hicho hapo. Hiyo ni kweli. Na mkifungue

nyumbani mwenu, ambako watoto wenu wanaweza kusikia kitu kifaacho.

53 Sasa, utasikia kila namna, bila shaka. Ni shughuli ya baina ya madhehebu, na namna yoyote ya mahubiri, ama yoyote. Huenda usikubaliane na baadhi ya hao ndugu, pamoja na mpango wao. Jamani, kama sisi sote tungaliketi chini kula usiku wa leo, na sote tulikuwa na sambusa, huenda nikachukua sambusa ya cheri, nawe uchukue tofaa, bali sisi sote tunakula sambusa. Sivyo? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, ninii tu, hao ni ndugu. Nao wana haki ya kueleza kile wanachofikiria.

54 Basi kwa hiyo idumishe redio yako ikiwa imefunguliwa, na uusikilize huo muziki mzuri. Nami na—nafikiri ni—ninathamini. La—laiti ningaliweza kuenda nayo nyumbani, KAIR, na kuiweka katika Louisville mahali fulani, kituo kama hicho, kinachotangaza muziki wa Kikristo wakati wote. Ninapenda hilo. Bwana na akibariki kituo hicho, KAIR.

55 Halafu basi, kuna kituo kingine huko nje. Sikumbuki he—herufi zake, lakini pia kina muziki mwingi mzuri wa kidini. Nami nawaambia; natumaini simwaibishi mtu huyo kwa kusema mimi humsikiliza Ndugu Gilmore wakati wote. Yeye yumo kwenye kituo hicho wakati mwingine. Nami ninasahau tu kituo hicho ni kipi. Lakini wao pia wana...KAIF? [Ndugu fulani anasema "La, KFIF."—Mh.]. KFIF. Hicho ni kituo kingine kizuri. Tunawathamini, pia.

56 Mnajua, ni kama tu ule msemo wa kale, kama tukihesabu baraka zetu, tuangalie kote, kwa namna fulani ni jambo la kushangaza kuona ni watu wangapi wazuri waliosalia ulimwenguni, na ni mambo mangapi mazuri tungali nayo. Bwana asifiwe. Nina furaha kuwa Mmarekani. Nina furaha, kama mmishenari, nikija kutoka nchi zingine, na kadhalika, na kuja nyumbani.

57 Loo, inanihuzunisha moyoni kuona jinsi, jinsi tunavyoishi kianasa, huku ulimwengu wote ukifa kwa njaa. Na—na kuona mahali pazuri, kanisa zuri kubwa kwenye kila pembe, na—na hao watu maskini huko, na wengi wao hata hawajalisikia Jina la Yesu Kristo.

58 Nilikuwa na maskini wavulana wadogo weusi waliosimama kwa maelfu, machozi yakitiririka mashavuni mwao, hata hawajavaa kipande kimoja cha nguo, hawajui ni upi mkono wa kulia na wa kushoto, wanakaa tu mchana wote na usiku kucha, wameketi pale, wakinisikiliza nikizungumza juu ya Bwana Yesu, mnaona, hawajasikia Hiyo hapo kabla. Waambie ya kwamba—ya kwamba kuna mtu anayewapenda. Loo, jamani. Hilo ndilo wanalotaka kusikia, kitu ambacho...mtu fulani anayewapenda.

59 Ni nani asiyetaka kupendwa? Sote tunataka hilo. Sote tunalihitaji. Halafu basi, jinsi ya kulipata, ni kufanya… kumpenda mtu mwingine, ndipo wewe utapendeka.

60 Mungu awabariki nyote. Ninatumaini kuwaona asubuhi kwenye kiamshakinywa, wale wanaoweza. Nami nafikiri watakuwa wakiuza tikiti ofisini asubuhi pia. Na kama ukija kwa ajili ya kiamshakinywa, mbona, nina hakika tutapata sukari ya rojorojo zaidi kidogo kama tukiwa na chapati maji. Halafu basi…Na labda wengine si kila mara wanahitaji nyingi hivyo, mwajua. Na kwa hiyo wakati mimi…

61 Wakati mmoja, nilikuwa nikihubiri kwenye kanisa la Baptisti ya Kimishenari huko chini Georgia. Ilikuwa ni… Nilihubiri ikafika usiku sana, kisha nikafanya wito mkubwa wa madhabahuni. Mimi…Muda ulikuwa umeenda. Na nilikuwa nikilala kwenye baraza la nyuma, huku upepo ukivuma ndani, maskini baraza la kale lenye kiambaza. Nami nilikuwa—nilikuwa nimechoka. Wao huamka, saa kumi, huko chini. Na kwa hiyo maskini mwanamke huyo mweusi akatokea. Akaniita, mara tatu ama nne. Nami kamwe silisahau hilo. Akasema, "Kasisi." Hilo linamaanisha "mhubiri," huko chini. "Kasisi," kasema, "mpenzi, kwa nini usiamke?" Kasema, "Nimekwishapika magole yako mara nne tayari." Nautakia heri maskini moyo wake. Alikuwa na umri wa karibu miaka sabini wakati huo. Nadhani ameondoka kwenda Utukufuni sasa, na kustarehe. "Nimepika magole yako mara nne, tayari, asubuhi ya leo."

62 Sasa, kila mtu anampenda Bwana? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nina furaha sana. Hivi huna furaha kujua, tu, unaweza kuwa huru, na kujisikia mwenye furaha, tena bila hukumu ya dhambi?

63 Pia ninataka kushukuru maskini kundi hili la waimbaji wanne hapa kwa kubaki huku. Ninajua walikuwa wamepangiwa mahali pengine. Na wakasema…Nitakuwa nikiwasikiliza, kwenye santuri zenu. Nina baadhi yake, na kanda, na kadhalika. Nafikiri ninyi ni wazuri sana.

64 Na maskini msichana huyu hapa. Jamani, loo, jamani! Yeye, yeye ni sehemu ya ndege mwigo. Hakika anaweza kuimba kweli, na hao wavulana wadogo, pia. Nami nilimwambia jamaa huyo mdogo, maskini jamaa huyo anayevaa miwani. Nilikutana naye hivi majuzi usiku, nami nikasema, "Mwanangu, utakuwa besi, moja ya siku hizi." Kidogo alicheka, na kuangalia juu ya hiyo miwani. Nikasema, "Kidogo ulishangaa jinsi nilivyosema hilo." Nikasema, "Vema, unasikika kama nyukikambi kwenye jagi sasa." Na Yeye akasisimkwa kutokana na hilo. Nao ni watu wazuri. Bwana awabariki.

65 Nafikiri nilimpata mama vizuri wakati niliposema hivyo. Vema. Nilikuwa na mama mwingine hivi majuzi usiku. Na mimi

nadhani huyu ndiye baba hapa nje mahali fulani. Mtu fulani alielekeza hapa kwa baba. Naam. Vema. Bwana ambariki. Nami ninatumaini njia zetu zitakutana tena mahali fulani maishani. Zisipokutana, tutafika langoni pale asubuhi ile. Hiyo ni kweli. Sasa, kabla ya sisi . . .

66 Baada ya kujieleza jinsi tumefanya, na mimi ninaamini kwamba furaha huendana na Wakristo. Sijawahi kuwa na huzuni kwamba nilikuwa Mkristo. Daima nina furaha mimi ni Mkristo. Na, loo, kengele za shangwe zimelia moyoni mwangu sasa kwa miaka thelathini na mitano tangu Yesu Kristo alipoingia moyoni mwangu. Kamwe sijaweza kuielezea. Ni furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu. Lakini sasa, tunapolikaribia Neno, hebu na tuweke tu kando maskini kicheko chetu, na—na hebu tuangalie moja kwa moja kwenye Neno sasa, kwa dakika moja tu.

67 Bwana Yesu, sasa Wewe tusaidie, tunapolisoma Neno. Pia jalia Roho Mtakatifu mkuu aliyetumwa awe Mwalimu wetu, aliyetumwa kutulea, na kutufundisha mambo na njia ya Mungu, mjalie Huyo aje sasa na kulichukua Neno, na kulikabidhi Hilo kila moyo kama tu tulivyo na haja. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

68 Sasa, kama mkitaka kuyageukia Maandiko ninayotaka kusoma, yanapatikana katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 14, na tutaanzia kwenye kifungu cha 22.

> *Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkutano.*
>
> *Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.*
>
> *Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi; maana* pepo *zilikuwa za mbisho.*
>
> *Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya* maji. (Ama samahani.) . . .*akienda kwa miguu juu ya bahari.*
>
> *Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.* Bali Yesu mara . . .
>
> *Mara Yesu alinena nao, akawaambia, Jipeni moyo ni mimi; msiogope.*

69 Sasa, kama nilikuwa niliite hili somo . . .Nami hujaribu kuziweka jumbe hizi ndogo rahisi na kama mchezo wa kuigiza, kusudi hawa jamaa wadogo waweze kuzifurahia. Nami ningeliita hili somo, hivi: *Msiogope*.

70 Maneno matatu, mimi huyatumia mara nyingi sana: *Unasadiki Jambo Hili*? na, *Njoo, Umwone Mtu*. Na ni mafungu madogo ya maneno matatu.

71 Na sasa ninataka kulitumia hilo kwa ajili ya fungu la maneno: *Msiogope*. Halafu basi kwa ajili ya somo, ninaenda kutumia hili, "Mkutano wa ushuhuda baharini."

72 Hapana shaka muda ulikuwa umeenda sana wakati wa alasiri. Jua lilikuwa karibu tu kutua; utusitusi ulikuwa unaingia; nao wote wamechoka na kudhoofika. Ilikuwa ni siku kuu kwa kundi hilo. Yule mvuvi mkubwa, mwenye misuli migumu, mwenye upara alikuwa akikisukuma chombo kwenye bahari ya Galilaya. Na wakati hatimaye alipoifanya gubeti kuelea, alipanda chomboni na kuketi chini kando ya ndugu yake, Andrea. Kiliitwa, katika Biblia, chombo.

73 Sasa, chombo sicho tunachokiita chombo siku hizi. Vyombo siku hizo zaidi sana viliendeshwa kwa makasia. Navyo vilikuwa na. . . Kinga zilikuwa juu, na hakika mawimbi makubwa yalikuja juu ya bahari kule mara kwa mara, na iliwabidi kuwa na pande ndefu. Na kwa kawaida watu wawili kwa kila kasia, wameketi upande mmoja wa chombo, na mwingine upande mwingine, na wakati mwingine, watu sita ama wanane walivuta chombo. Walikuwa ni wavuvi wa biashara huko Galilaya. Nao wanayo leo hii. Haijabadilika hata kidogo tangu siku hiyo. Ingali ni vile vile, wanavua samaki vile vile, nyavu za aina ile ile, na kila kitu.

74 Sasa, na wakati walipokigeuza kile chombo na kuanza, ufuko ulijaa watu. Na wao wangepiga makasia mara kadha kwa makasia yao, na kuwaaga kwa kuwapungia mkono. Ndipo kila mtu anasema, "Rudini mkatuone tena. Hakikisheni kumleta Bwana wenu mtakaporudi kutuona tena." Walikuwa wakienda zao kuvuka bahari, na ilikuwa kidogo ni mbali. Na ingewabidi kuvuta kwa nguvu kuvuka kufika kule usiku huo.

75 Kwa hiyo ninaweza kuwazia kwa njia moja jinsi walivyojisikia. Ilikuwa ni siku kuu. Walikuwa wameona tamasha kuu zikifanywa. Wengi walikuwa wameokoka na kumwamini Bwana Yesu. Nao walikuwa wamekuwa na siku ngumu sana, kuwazuia watu wasimkaribie Bwana wao, ili aweze kuwahudumia, kuleta Uzima kwa waliopotea. Nao walikuwa wamechoka na kudhoofika.

76 Lakini, hata hivyo, kuwaacha marafiki zao, kuna jambo fulani kuhusu kuwaacha marafiki, wakati inapokubidi kusema kwaheri. Hilo ni—hilo ni jambo baya sana. Nami ninajisikia hivyo, naweza kuhisi kiasi hicho cha mzigo waliokuwa nao, kwa sababu ninajua jinsi ilivyo na mimi. Yapata wakati unapoanza kufahamiana na kundi la watu, wakati tu wanapoanza kujua ya kwamba wewe si mwanadamu maalum, wewe ni ndugu. Na—nao wakaanza kuninii. . . Kila kitu kinaanza kuleta hisia

nzuri. Ndipo inakulazimu kusema, “Kwaheri. Ni—nitawaona tena wakati mwingine. Ninatumaini kuwaona.” Hilo ni jambo gumu kufanya.

77 Ninautazamia wakati ambapo tutakutana ambako kamwe hatutasema kwaheri, huko kwenye Ng’ambo ya pili. Na baadhi ya ndugu zangu wazee hapa na wawindaji wenzangu, nita—nitakutana nanyi huko chini kwenye miburuzo mikubwa ya wanyama huko nyuma mahali fulani, ambako haiishi. Nitakuwa nikiwatazamia kule barabarani, nisiporudi kuwaona tena kabla hatujachukuliwa.

78 Na jinsi ambavyo hapana shaka walipunga mikono. Nao wangepiga makasia machache, na halafu wapunge mikono tena. Ndipo hatimaye, wakati bahari ilipotulia, wakati tu jua likitua, maskini kile chombo kikipenya kuvuka, kwa nguvu za makasia. Wangepiga machache, na kisha wapunge mikono yao, na kwaheri. Halafu basi—basi mtu mwingine angemtambua mtu mwingine, unawaaga kwa kuwapungia mkono. Na hapana shaka hivyo ndivyo chombo hicho kilivyokuwa kikienda humo majini. Na hatimaye, kwaheri ya mwisho ilisemwa, kadiri wanavyoweza kusikia.

79 Basi hapana shaka palikuwapo na kimya kirefu. Hakuna mtu aliyesema chochote, kwa sababu iliwabidi kukisukuma mbele maskini chombo hicho. Na kwa namna fulani walikuwa na mdundo wa namna fulani, wakati wanapovipiga vyombo hivi makasia wote pamoja, kwa sababu ungekipindua kama hukufanya hivyo. Na kwa hiyo walikuwa wakipiga makasia kwa uwiano, na huenda walikuwa wamechoka sana.

80 Hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana ambaye kwa namna fulani aliachilia kwanza, naye alitaka kupumua, kama tusemavyo. Yeye alikuwa ni mbichi na mwororo bado. Naye hakuwa na nguvu kama hao wavuvi wagumu waliokuwa baharini, na dhoruba, walikuwa wamevuta mitumbwi hiyo. Ndipo hapana shaka alichoka kwanza. Kwa hiyo hapana shaka alisema, “Whwiu, ndugu zangu, hebu tupumzike tu kidogo.” Ndipo wakati aliposimama, na kuzirudisha nywele zake nyeusi nyuma kutoka kwenye macho yake, nacho maskini chombo hicho kilikuwa kikisairi majini, kikisonga mblele, ninaweza kumsikia akianza na kusema, “Ninajisikia kama ningetaka kushuhudia.”

81 Na—napenda hilo. Ninapenda mkutano mzuri wa ushuhuda wakati ukiwa na kitu cha kushuhudia. Sasa, ikiwa huna chochote, unasimama tu na kusema jambo lile lile ulilosema majuzi usiku na mwaka jana, hilo huchosha. Bali unapokuwa na ushuhuda halisi mpya ambao huwezi kamwe kuushikilia zaidi, Bwana amekufanyia jambo fulani, nawe huna budi kulielezea, napenda hilo.

82 Tulikuwa tukiuita, nyumbani, ushuhuda wa bisi. Sasa, ni wangapi wanaojua bisi ni nini? Ninataka kuwaambia kile

ifanyacho. Unachukua punje ndogo ya manjano, na kuiweka juu ya jiko lenye joto, nayo inaruka juu sana hewani ikiwa manjano, inageuka nyeupe, inarudi ikiwa mara mbili ukubwa wake na nusu nyepesi, nusu uzito wake, hasa, kama ilivyokuwa. Ni ushuhuda. Mnaona? Hicho ndicho ushuhuda ufanyacho. Maskini manjano, anayeogopa kufanya lolote, halafu basi, muda si muda wajua, nguvu na moto wa Roho Mtakatifu unakupiga na kukufanya mweupe, kutoka manjano. Nawe unajisikia mwepesi sana, unaniii tu, unaona, hujatiwa nanga ardhini tena. Kwa hiyo ninapenda ushuhuda wa bisi.

83 Hapana shaka ilikuwa ni maskini Yohana aliyetaka kutoa mmoja. Aliinuka kwenye mtumbwi na kusema, "Vema, ninataka kushuhudia kwanza, na kusema hivi wakati tukipumzika. Nimeridhika kikamilifu na kuhakikishiwa, ndugu zangu. Leo hii ilitatuliwa moyoni mwangu kwamba sisi hatufuati namna fulani ya shupavu wa dini, kama ulimwengu wote unavyotaka kutufanya tuamini tunafuata. Tunamfuata Yeye ambaye Maandiko yalinena habari Zake. Limetatuliwa leo hii. Ninataka kutoa ushuhuda wangu."

84 "Nilizaliwa na kulelewa karibu na Yordani. Ninaweza kukumbuka, miaka mingi iliyopita, wakati nilipoishi kwenye kingo za Yordani, karibu tu na kivuko ambapo Israeli walivukia pamoja na yule shujaa mashuhuri, Yoshua. Alichukua lile sanduku la agano, ndipo Roho Mtakatifu akaifungua bahari, ninii . . . ama Yordani, nao wakavuka wakapita, watu wetu wote, juu ya nchi kavu, tulipoingia kwenye nchi hii.

85 "Ninakumbuka, kwenye majira ya kuchipua, jinsi nilivyokuwa nikitoka nje na kuchuma maua madogo kwenye u—ukingo wa Yordani. Na kwenye, alasiri, ninaweza kumsikia mama yangu akiniita, bado, na kusema, 'Sasa, ingia, Yohana. Na wewe—wewe huna budi kwenda kitandani. Inakupasa kulala kidogo. Wavulana wadogo hawana budi kulala kidogo wakati wa alasiri.' Naye angeketi kwenye baraza la mbele, na kunipembeza mikononi mwake. Nami ninaweza kuuona uso wake mrembo, bado, wakati macho yake makubwa ya Kiyahudi, marembo, ya hudhurungi yalipoinama yakanitazama. Naye angenisimulia hadithi za Biblia."

86 Na, mwajua, ni vibaya sana kwamba mama zetu hawawezi kukaa mbali na kilabu cha pombe muda mrefu kutosha, leo hii, na mbali na mahali wasipopaswa kuwapo, na kuwapembeza watoto wao tena na kuwasimulia hadithi za Biblia. Hiyo ndiyo shida ya taifa letu leo hii. Wao, wowote, karibu, mtoto yeyote mtaani anaweza kukwambia zaidi juu ya Davey Crockett kuliko wanavyoweza juu ya Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Na jinsi ulimwengu wa kibiashara unavyoyachukua hayo! Na, jamani! "Mlee mtoto katika njia impasayo." Ni kweli.

87 Sasa, "Naye," kasema, "alikuwa akiniambia hadithi. Na

moja ya hadithi muhimu niliyopenda kuliko zote, ilikuwa. . . Isitoshe, yule mvulana mdogo ambaye yu—yule nabii mashuhuri Eliya alimfufua kutoka kwa wafu, nilikuwa ninaipenda hadithi hiyo, na kushangaa Eliya alikuwa ni mtu wa namna gani. Naye angeniambia, 'Unajua nini, Yohana? Eliya yuyo huyo mashuhuri na Elisha, wote wawili, walitembea moja kwa moja kwenye barabara ile pale, wameshikana mikono, wakishuka kwenda mtoni. Wazia tu, si muda mrefu uliopita walifanya hivyo. Hao manabii wawili mashuhuri walishuka wakaenda mtoni, nao mto ukafunguka. Wakapitia moja kwa moja karibu na Yeriko.'"

88 Sasa, "Lakini hadithi muhimu ambayo daima ilidumu nami, ambayo aliniambia, ninataka anisimulie kila siku, jinsi ambavyo kwamba Mungu aliwatoa watu wetu kutoka utumwani huko Misri ambako walikuwa watumwa, na akawaleta nyikani, na kuwaweka huko nje miaka arobaini, na kuwalisha kutoka Mbinguni. Mbona, yeye aliniambia hiyo, kila usiku, kwamba wangetoka nje asubuhi baada ya Israeli wote kuingia kitandani na kulala, kama vile alivyokuwa akijiandaa kunilaza kitandani. Mnajua nini? Kasema Yehova Mungu alishuka, na kesho yake asubuhi kulikuwako na mikate kote ardhini. Hiyo ingewatosha siku nzima.

89 "Nami nilikuwa nikimwambia Mama, 'Mama, hivi Mungu ana kundi maalum la Malaika huko juu, wanaofanya kazi usiku; na analo lundo kubwa la tanuri kote Mbinguni, na Yeye angeninii, "Sasa, hima sasa, watoto hawa wana njaa; na kuoka mikate hii yote"? Kisha kundi lingine la Malaika wanaishusha chini na kuiweka kote sakafuni'?

90 "Angeniangalia, na kusema, 'La, Yohana, kipenzi. Wewe ni mvulana mdogo tu. Huelewi. Yehova wetu mkuu ni Muumba. Haimbidi kuwa na Malaika maalum kuoka mkate. Hahitaji tanuri lolote Mbinguni. Yeye hunena tu Neno, nayo mikate inaanguka kote ardhini. Yeye ni Muumba.' Nami nisingeweza kuelewa jinsi hiyo ilivyokuwa. Bali hadithi hii daima ilidumu nami, kwa namna fulani.

91 "Nami nimemwangalia Bwana wetu katika mambo mengi, ya kuwaponya wagonjwa, na kadhalika. Lakini, leo hii, ndugu zangu, nilipomwona akizichukua zile biskuti tano na wale samaki wawili, kutoka kwa yule mvulana mdogo ambao walikuwa ni chakula cha mchana, aliyekuwa amekwepa shule. Nilipomwona akiwachukua hao, na kusema, 'Wafanyeni, watu waketi chini hamsini-hamsini.' Mara nilipowaketisha hamsini wangu chini, nilipanda juu kwenye mwamba ule na kuangalia, nione kile Yeye angefanya. Ndipo alipochukua kipande hicho, mkate boflo, akamega nusu kutoka kwake, na kuiweka kwenye sahani, na kufikia wakati alipourudisha mkono Wake tena, kulikuwako na nusu boflo nyingine ya uliovunjwa. . .mkate uliookwa.

92 "Sasa, kuna uhusiano fulani kati Yake na Yehova, maana alikuwa akiumba mkate huo na samaki huyo, papo hapo mbele yangu. Hakuna yeyote mwingine angaliweza kufanya hivyo ila Yehova. Na huyo ni Mungu yeye yule ambaye mama yangu aliniambia kumhusu, nyikani huko nyuma, Yule ambaye alishusha chini mkate, kutoka kwa uumbaji, kutoka Mbinguni. Sisi, kwa macho yetu wenyewe, tumemwona Yeye leo akiumba mkate moja kwa moja mbele zetu."

93 Uliwahi kuwazia ni atomu ya namna gani iliyomlazimu Yeye kuachilia? Unga ulitoka wapi? Sio unga tu, bali ulikuwa tayari umeokwa kuwa boflo na tayari kuliwa. Alikuwa na samaki. Alikuza samaki kwanza. Lakini sasa anavunja samaki, nusu, mara mbili, na samaki mwingine angekulia pale, bali samaki huyu anayetokea pale amepikwa tayari na kuokwa, na kukuzwa, pia. Alifanya nini? Loo! Yeye ni Mungu. Ananena tu, hayo ndiyo yote yanayompasa Yeye kufanya. Yeye ni . . . Ni . . .

94 Sasa, mvulana huyo mdogo, chakula hicho kidogo cha mchana alichokuwa nacho, hakikuwa kingi sana mikononi mwake, lakini wakati alipoachilia kile alichokuwa nacho kiingie mkononi mwa Yesu, kililisha maelfu. Na labda imani iliyo ndogo . . . Unasema, "Vema, laiti ningalikuwa na imani kubwa." Lakini imani hiyo ndogo uliyo nayo . . . Unayo imani ya kutosha kuja kanisani. Halafu basi, kama una imani kiasi hicho, mbona usiiweke tu mikononi mwa Yesu, nayo itawalisha maelfu. Ikiwa wewe . . . Hakuna nyingi mikononi mwako. Lakini mara ikiwa mikononi Mwake, basi itafanya miujiza kama ukiiacha imani hiyo ifike mikononi Mwake.

95 Angalia. Basi Yohana alikuwa amesisimkwa kabisa. Ninamsikia Andrea akisema, "Ngoja kidogo, mwanangu! Usisukesuke mtumbwi huo namna hiyo. Chukua wakati wako. Usishtuke sana juu ya jambo hili, wajua. Hata hivyo, tuko huku nje kwenye bahari hii."

96 "Vema, hufurahisha tu moyo wangu kabisa," akasema, "kuona, na kujua ya kwamba—ya kwamba Mungu amejifunua Mwenyewe kwetu hapa, Mtu tunayeweza kumgusa. Yeye ni—Yeye ndiye . . . "

97 Si ajabu, nabii alisema Yeye angekuwa Imanueli, kwamba Mungu angewakilishwa hapa ndani Yake. Nasi tunamwona Yeye akifanya kazi zile zile ambazo Baba alifanya. Si ajabu Yeye angeweza kuwaambia hao Mafarisayo, 'Kama Mimi . . . Ni nani anayeweza kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi? Ni nani anayeweza kunishtaki Mimi? Kama kila kitu Biblia ilisema kwamba nitafanya, kama sijakifanya!'"

98 Mwajua, dhambi ni kutokuamini, mwajua. Hivi mlijua kusema uongo si dhambi? Kufanya uzinzi, hiyo si dhambi. Kunywa wiski, kuvuta sigara, kulaani, kulitumia Jina la Bwana,

hiyo siyo, hiyo si dhambi. Hizo ni sifa za kutokuamini. Unafanya hivyo kwa sababu wewe si mwaminio. Kuna dhambi moja tu.

99 Nilisema hivyo usiku mmoja katika kanisa la Kimethodisti. Ndipo maskini dada aliyesimama pale, mwajua, ukosi wake umesimama wima, akasema, "Kasisi Branham, naomba uniambie, dhambi ni nini?"

Nikasema, "Kutokuamini." Hiyo ni kweli.

100 Unafanya hivyo kwa sababu wewe ni asiyeamini. Kama ukifanya hivyo, ungali ni asiyeamini. Hiyo ni kweli. Kuna mambo mawili tu: ama wewe ni mwaminio, au si mwaminio. Kwa hiyo basi Biblia ilisema, "Asiyeamini amehukumiwa tayari." Mnaona? Kwa hiyo dhambi ndilo jambo pekee, ambalo ni matokeo ya kutokuamini.

101 Naye Yesu alisema, "Ni nani awezaye kunihukumia kutokuamini? Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Bali nikizitenda hizo kazi, na hata hivyo hamwezi kuniamini, aminini kazi nizifanyazo." Kwa hiyo, mnaona, hapa Yeye alikuwa akifanya jambo lile lile alilofanya Mungu.

102 Sasa ninataka kuwaulizeni, ndugu zangu. Kama Uhai wa Yesu Kristo uko ndani ya Kanisa, basi hakika Kanisa linapaswa kufanya jambo lile lile Yeye alilofanya, kwa sababu Uhai ule ule uko ndani Yake.

103 Kama hapa unasimama mpichi, nami nitoe uhai wote wa pichi kutoka kwake, na kuweka uhai wa tofaa ndani yake, utazaa tunda la namna gani? Matofaa. Hiyo ndiyo aina ya uhai ulio ndani yake.

104 Vema, basi, kama Uhai uliokuwa ndani ya Kristo uko ndani yetu, Huo utazaa matunda aliyozaa Yeye. Hauna budi kuzaa.

105 Basi ni m—ni mchanganyiko jinsi gani walimoingia watu, leo hii, ambao, wanawazia kwamba, kwamba Ukristo ni moja ya vitu dhaifu kuliko vyote. "Yote wafanyayo ni kuandika jina lao kwenye kitabu, na kumfanya mtu fulani kuwanyunyizia, ama kitu kingine, na kumpa mhudumu mkono wa kuume wa ushirika. Na hayo ndiyo yote. Wanaondoka tu." Huo si Ukristo.

106 Ukristo ni kujikana mwenyewe. "Uchukue msalaba wako kila siku. Mfuate Yeye." Kufa, kwa mambo ya ulimwengu. Wakati hukumu yote imeondoka, "Hakuna basi sasa hukumu ya adhabu kwao walio katika Kristo Yesu." Unaingiaje ndani Yake? Kwa kujiunga? La. Kupeana mikono? La. Kwa muungano? Kwa elimu? "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja." Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu sisi tuko ndani ya Kristo. "Basi hakuna hukumu ya adhabu kwao walio ndani ya Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali kwa kufuata mambo ya Roho." Amina. Loo, hilo, hilo lingemfanya mtu yeyote kupaza sauti. Amina. Kuwa mle ndani, kwa vyovyote vile, hiyo ndiyo sehemu nzuri. Vema.

107 Sasa tunaona hapa, kwamba, katika jamaa aliyefuata kusimama kushuhudia, lazima alikuwa ni Petro. Ninaweza kumsikia akisema, "Naweza kutoa ushuhuda wangu baada ya huyo?"

108 Mwajua, unapokuwa na jambo fulani la kushuhudia, karibu tu huna budi kupata ruhusa, kwa sababu kuna kuenenda kwelikweli. Nao mkutano huu wa ushuhuda ulikuwa ukiendelea. Maskini mtumbwi ule ukisukasuka tu, nao hao ndugu wakipigapiga tu miguu yao chini na kuwa na wakati mzuri kule nje. Laiti ningalikuwa kule nje! Hivi si ungetaka kuwa kule nje na kuusikiliza ushuhuda huo? Ilibidi maskini Yohana kuketi chini. Alikuwa amesema yote aliyoweza wakati huo.

109 Simoni akasimama. Akasema, "Mwajua, wakati Andrea alipoanza kwenda kule chini kwa mtu huyo, ambaye nchi ilidhani alikuwa namna fulani ya mtu wa mwituni, huyo Yohana, kanisa lilidhani alikuwa ni mtu aliyerukwa na akili. Hata hivyo, baba yake alikuwa ni kuhani. Naye. . .Mwajua, ni kawaida miongoni mwa watu wetu, kwa mwana kufuata chochote baba alichofanya. Bali, mnajua, kazi yake ilikuwa ni kuu sana. Badala ya kushuka kwenda kule kwenye hiyo shule yote kubwa, na kushindiliwa na hayo; hu—huduma yake ilikuwa ni kuu mno. Mungu alimpeleka huko nje nyikani, na kwenye umri wa miaka tisa.

110 "Naye akajionyesha mwenyewe tena kwenye umri wa miaka thelathini, kwa sababu huduma yake ilikuwa ni kumtambulisha Masihi. Naye huyo Masihi alikuwa awe na ishara, naye ilimbidi kujua ishara hiyo ilikuwa ni gani. Kama angeshuka kwenda huko na kudungwa baadhi ya mambo haya ya kimadhehebu, mbona, mtu fulani, askofu fulani mkuu angesema, ama kuhani mkuu mashuhuri angalisema, 'Sasa, angalia hapa, Yohana, tunajua ya kwamba uta—utamtambulisha Masihi, kama ilivyosemwa na—na Malaika. Nawe utamtambulisha. Hivi hudhanii kwamba Ndugu *Nanii* hapa anakidhi hiyo—hiyo tikiti vilivyo kikamilifu?' Huenda angekubaliana nalo. Lakini, mnaona, alijitenga mwenyewe na kila kitu, ili aweze tu kusikiliza na kuona kile Mungu alichosema juu yake."

111 Nami nafikiri hilo ni somo zuri kwetu usiku wa leo. Kama tutajitenga wenyewe na mafundisho haya ya sharti ya kujibunia na kanuni za imani, na kadhalika, na kuangalia katika Biblia na kuona yale Mungu aliyosema juu yake. Anapaswa kujua kilicho sahihi. Ni Neno Lake, Kitabu Chake. Hiyo ndiyo sababu ninapenda Injili yote, sio nusu yake; yote, Injili yote.

112 Sasa, na ndipo—ndipo akasema, "Jambo la kwanza, mwajua, huyu hapa Andrea anakuja mbio, na anasema ya kwamba mhubiri huyu alisema aliiona ishara ya Masihi juu ya Mtu fulani. Ilikuwa ni Nu—Nuru, kama hua akishuka, na—naye mhubiri

huyo akaiona. Na kulikuwako na wengi kule, na hakuna mtu mwingine aliyeiona ila yule mhubiri. Kwa hiyo ilikuwa vigumu kwangu kuendea hilo. Ninasikia kila namna ya upuuzi, kwa hiyo nilisahau tu hayo, mwajua. Ndipo usiku mmoja akanijia, kasema, 'Unapaswa kwenda tu huko chini ukamsikilize Huyo angalau mara moja. Atakuwa hapa chini ufukoni kesho asubuhi, nawe unapaswa kushuka uende huko.'

113 "Vema, nikawazia, 'Maskini mzee Andrea. Mimi na yeye tumeuvuta mtumbwi huu muda mrefu.'

114 "Pia ninakumbuka siku moja nilikuwa na mazungumzo na baba yangu. Naye alikuwa mzee mzuri, Mfarisayo. Yeye aliishi tu kwenye kanisa hilo; nguzo ndani yake. Na nywele zake zenye mvi! Usiku mmoja baada ya kuvua samaki . . .

115 "Tulikuwa maskini. Ilitubidi tu kuishi kimaskini tulivyoweza. Na mara nyingi, wakati mama na baba walikuwa hai, alikuwa anatukusanya sote asubuhi, kabla hatujatoka kwenda kuweka nyavu zetu majini. Tulikuwa na madeni, na ilitubidi tupate samaki. Nasi tungemwomba Yehova, ku—kuzijaza nyavu zetu siku hiyo. Na jinsi baba angeshangilia tulipopata mvuo mkubwa mno wa samaki; kisha tunarudi ufukoni, na kutoka nje ufukoni, na kuketi chini na—na kumshukuru Mungu kwa kutupatia samaki kwa ajili ya siku hiyo. Jinsi ambavyo tungeenda kulipa madeni yetu sasa, na kupata chakula cha usiku huo, na kutarajia kesho yake asubuhi!

116 "Basi usiku mmoja, baada ya sisi kumaliza kumshukuru Bwana, ninakumbuka baba aliketi chini kando ya demani ya mtumbwi. Kisha akaniita pale, naye akasema, 'Simoni, unajua, nimetamani, maishani mwangu mwote, kuishi kuiona siku ambapo ningemwona Masihi. Nasi tumeahidiwa Yeye, kwa miaka mingi. Watu wetu wote wamemtarajia. Musa alitwambia Yeye alikuwa yuaja. Manabii wote wamezungumza na Yeye. Lakini, Simoni, mwanangu, hatujakuwa na nabii miongoni mwetu kwa mamia ya miaka. Na wakati kanisa limeenda kombo katika hali baridi, ya kawaida, bali ninaamini wakati huo umekaribia. Ukiona mvi wangu . . . Sidhani nitaishi kuliona. Mimi ni mzee sasa.'

117 "'Lakini, Simoni, kabla Masihi huyo hajaja, Shetani atatuma upuuzi mwingi wa uongo, kwanza, na watakuja masihi wa uongo. Ila nakutaka daima ukumbuke, Simoni, kamwe usiliache Andiko hili. Watu wetu wameambiwa katika Biblia hii, kwamba, "Neno la Bwana humjia nabii, nabii pekee." Halafu basi, kwanza, nabii huyu hana budi kuthibitishwa na Mungu. Hana budi kulisema Neno, na hilo Neno halina budi kutimia, wakati baada ya wakati.'"

118 Wanazaliwa. Hao si mtu tu kuwawekea mikono na kuwafanya nabii. Wanazaliwa. Kuna karama ya unabii inayoweza kuja, bali nabii anazaliwa nabii. Yeremia alikuwa

hivyo. Mbona, Mungu alisema, "Kabla hata hujaumbika katika tumbo la mama yako, nilikuchagua nabii juu ya mataifa." Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na mbili kabla hajazaliwa, Isaya alisema, "Yeye ni sauti ya mtu aliaye nyikani." Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, kabla ya msingi wa ulimwengu. Alikuwa ndiye Uzao wa mwanamke aliyekuwa akiponde kichwa cha nyoka. Hakika.

119 Mungu yuko. Mungu huyaweka mambo haya. "Mungu ameweka Kanisani mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti." Mambo haya yote, Mungu aliyaweka Kanisani. Halafu kuna karama tisa mbalimbali ambazo zinafanya kazi katika Kanisa hilo. Bali hizi ni ofisi zinazoingia Kanisani.

120 "Na wewe unajua, yeye aliniambia, kasema, 'Mwanangu, tumemfuata Musa na torati zake. Sasa, Musa alitwambia kwamba Masihi huyu, atakapokuja Yeye, atakuwa ni nabii.'

121 "Kwa hiyo niliwazia tu ningeshuka niende nikaone Jamaa huyu kijana alikuwa ni nani, anayechochea mhemuko huu wote huko chini." Kisha kasema, "Watu wanaponywa na Yeye, kwa hiyo niliwazia ningeshuka niende huko. Basi siku moja wakati tulipoziosha nya—nyavu zote na kuzianika nje ufukoni, Yeye alishuka akaja kuhubiri. Basi nikajipatia kipande kimoja, na kuketi juu ya ubao uliopwelewa, huko ufukoni. Basi alipoanza kuzungumza, ni—nilijua ya kwamba kulikuwako na kitu fulani tofauti kumhusu Mtu huyu, kwa sababu Yeye alizungumza kama Mtu aliyefahamu yale aliyokuwa akizungumzia.

122 "Basi nilipomkaribia, Yeye alinikazia macho usoni, ndipo akasema, 'Jina lako ni Simoni, na wewe ni mwana wa Yona.'" Akasema, "Hilo lilichukua. . .Hilo lilitosha kwangu. Sio tu kwamba alithibitisha kuwa ni Nabii, Yeye alinijua kabla hajaniona. Alinijua, na pia alimjua maskini yule baba yangu mzee mtauwa, ambaye aliniambia hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi. Hilo lilitosha kwangu." Loo, jamani! Jinsi alivyokuwa akisisimkwa sana, pia!

123 Na hapana shaka ilikuwa ni Filipo aliyeruka juu, yapata wakati huo, kasema, "Naomba nishuhudie. Ngoja kidogo. Hebu mimi, hebu niseme jambo fulani." Kasema, "Sasa, Ndugu Nathanaeli, usione haya." Akasema, "Nilikuwa nimesimama hapo wakati huo, ndugu zangu, kama nyote mnakumbuka. Nami nikaona hilo likitendeka. Nami nikajua hiyo ilikuwa ndiyo ile iliyokuwa—iliyokuwa ishara ya Masihi. Nanyi mwajua, haikuwa ni muda mrefu sana tangu mimi na Filipo, pale, tulikuwa tukisoma hayo katika Maandiko. Kwa hiyo nikakimbia kuuzunguka mlima, kule yapata maili kumi na tano, na kumwambia, nikampata Filipo chini ya mti, akiomba. Basi nikasema, 'Filipo, njoo umwone Yule tuliyempata, Masihi, na Yule ambaye Musa alinena kumhusu; na Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.' Basi, Nathanaeli, unakumbuka uliyosema?"

"Naam, ninakumbuka. Hakika ninakumbuka."

124 "Ulisema, 'Laweza Neno lolote jema kutoka Nazareti sasa?' Nami nikasema, 'Njoo, uone.' Basi tulipozunguka kule, unakumbuka tukizungumza? Nami nilikuambia kuhusu Yeye kumwambia Simoni hivyo, na nikakwambia kwamba huenda Yeye akakwambia wewe ni nani. Nawe ukaenda kule juu, kasema, 'Sasa, itanibidi kuona hilo, ili kuamini.' Pia unakumbuka jinsi ulivyotembea, mikono yako ikiwa nyuma yako? Na mara ulipofika Uweponi Mwake, unajua lililotukia?"

"Hakika ninajua."

"Alisema, 'Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.'"

125 "Nami nakumbuka jinsi hilo lilivyokushusha. Nawe ukasema, 'Rabi, ulinijua lini Wewe? Na mimi hapa. Ndio kwanza niletwe kwenye mkutano huu. Basi ulipataje kamwe kunitambua? Hujawahi kuniona, maishani Mwako. Ungewezaje kunijua Wewe?' Akasema, 'Mbona, kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.' Loo, ninakumbuka uliyosema. Ukaenda Kwake mbio na kusema, 'Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.'"

126 Hapana shaka ilikuwa ni Andrea aliyesema, "Sasa ni wakati wangu kushuhudia. Mnakumbuka ule wakati ambapo sisi—sisi tulidhani tulikuwa tukishuka kwenda Yeriko? Nasi tunajua, huko chini Yeriko, jinsi ambavyo yule mzee kipofu alivyotoka huko siku hiyo. Naye alikuwa. . . Hata tusingeweza kumsikia akipiga yowe. Alikuwa akipiga makelele, akiendelea. Ndipo—ndipo imani yake ikamsimamisha Bwana wetu, naye akafunguka macho.

127 "Nanyi mnakumbuka huko Samaria, tuliposimama kule juu, kushuka kwenda kununua chakula? Basi—basi tulipokuwa tumeondoka. . . Tulitaka Yeye aambatane nasi na kununua chakula, na Yeye asingekuja. Asingeenda kamwe. Yeye alisema, 'Mimi ninacho chakula msichojua chochote kukihusu.' Kwa hiyo wakati sote tuliporudi nyuma, tulimwona Yeye akizungumza na mwa—mwanamke mwenye sifa mbaya. Alikuwa ametiwa alama. Nasi tukawazia, 'Bwana wetu anafanya nini kule juu kisimani, akizungumza na mwanamke huyu mwenye sifa mbaya?' Kwa hiyo mnakumbuka, tulinyemelea pale, karibu, nyuma ya kichaka, tukasikiliza yale waliyosema. Ndipo Yeye akamwambia mwanamke huyo, 'Mwanamke, nipe maji ninywe.' Nasi tulishangaa, kuwazia ya kwamba Bwana wetu angezungumza na mwanamke wa namna hiyo." Mnaona?

128 Hao hawakuwa wameongoka kikamilifu. Tungali tuna wa aina hiyo leo hii, wanaowazia ya kwamba Mkristo hapaswi kuzungumza na mlevi ama kahaba. Huyo ndiye mtu wanayepaswa kuzungumza naye. Huyo ndiye mtu wanayepaswa.

Huyo ndiye mtu aliye chini. Huyo ndiye mtu wa kuinua. Huyo ndiye anayemhitaji Mungu.

129 "Kwa hiyo tukamsikiliza, na—na mazungumzo yakaendelea. Na hatimaye Yeye akamwambia mwanamke huyo, 'Nenda, kamwite mume wako mje naye hapa.' Naye mwanamke akasema, 'Sina mume yeyote.'"

130 Ndipo Andrea akasema, "Mnakumbuka jinsi sisi sote tulivyotazamana? 'Jamani, mara moja Yeye alipokuwa amekosea! Kuna kuteleza, mahali fulani, kwa sababu hapa Yeye anamwambia, "Nenda, kamlete mumeo," naye anajibu, "Sina mume yeyote." Na Yeye anamwambia, "Umesema kweli."' Ndipo sisi sote tulishangaa. 'Tulikuwa tunaenda kusema nini sasa? Sasa Yeye amemwambia mwanamke huyo ana mume; naye anageuka, anasema hana mume. Naye huyu hapa Bwana wetu, nayo hii hapa ile ishara ya Masihi ambayo tulipaswa kuitazamia, nayo hapa imeshindwa.' Nasi tulishangaa, mmoja kwa mwingine, huku tukitazama.

131 "Ndipo basi Yeye akasema, 'Umesema kweli. Kwa sababu, una waume watano. Na yule uliye naye sasa, na unayeishi naye, siye mume wako.' Nanyi mnakumbuka jinsi huyo mwanamke alivyomwangalia na kusema, 'Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii'?"

132 Sasa, li—li—lile baraza kuu la makanisa ulimwenguni siku hiyo, walipoangalia hilo, walisema, "Mtu huyu ni mpiga ramli. Mtu huyu ana pepo. Yeye ni Beelizebuli." Mngewazia ya kwamba viongozi wa dini wangeweza kuchukua wazo kama hilo, usoni pa wakati ambao lilipaswa kutukia, na kulingana na Maandiko? Lakini walilichukua. Na wangali wanafanya hivyo. Sasa, wao walisema, "Ni, loo, ni roho ovu juu ya Mtu huyu. Hivyo ndivyo Yeye anavyofanya. Yeye ni—Yeye ni Beelizebuli tu. Hivyo ndivyo ilivyo."

133 Bali maskini mwanamke huyu, mwenye sifa mbaya alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii."

134 Alijuaje kwamba Yeye alikuwa ni nabii? Kwa sababu Yeye alimwambia kitu fulani kilichokuwa maishani mwake, kasema, "Wewe ni nabii."

135 Naye akasema, "Sasa, tunajua, sisi Wasamaria, tunajua kwamba ajapo Masihi, anapaswa kufanya mambo haya. Yeye hutwambia mambo yote."

Ndipo Yesu akamwangalia usoni na kusema, "Mimi Ndiye."

136 Basi hilo lilitosha. Hapakuwapo na swali tena. Ishara ilikuwa imetolewa. Yeye alikuwa ameipokea. Yeye alijua hilo. Akaangusha mtungi wake wa maji, naye huyo akaingia mjini.

137 Sasa, kulingana na desturi; na mtu yeyote ambaye amesafiri, anajua hili. Hakupaswa kufanya hivyo. Hiyo ni kukiuka maadili kwa mwanamke huyo mwenye sifa kama hizo, mwanamke wa—

wa aina hiyo, kusema lolote kwa mwanamume mtaani. La, bwana.

138 Lakini nini? Alikuwa amepata kitu fulani. Alikuwa kama nyumba inayowaka moto, kwenye siku yenye upepo. Usingeweza kumnyamazisha. Alikuwa amepata kitu halisi. Akakimbia kupitia mtaani, akisema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi Mwenyewe?" Amina. Mungu na atupe waongofu wengine kama hao. "Mnajua tunamtazamia Masihi," wakasema. "Tunamtazamia Yeye. Na pale ameketi Mtu moja kwa moja pale kisimani sasa, aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini hiyo ndiyo ishara yenyewe ya Kimasihi tunayopaswa kutazamia?"

139 Ndipo wakamleta mjini. Kamwe hakulifanya mara nyingine tena. Lakini Biblia ilisema kwamba watu wa mji huo walimwamini Yeye kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo. Amina. Jinsi Mungu anavyoweza kufanya mambo! Waliamini. Naye Mtu huyu hakuwa amewahi kuwa katika mji huo hapo kabla, na anasimama pale na kumwambia mwanamke huyo alikuwa na waume watano. Nayo ilikuwa ni kweli. Na ilikuwa ni saa, na wakati, nao wakaiamini.

140 Kwa nini hatuwezi kuamini? Kwa nini Tucson haiwezi kuamini? Kwa nini ulimwengu wa kanisa hauwezi kuamini? Kwa nini Marekani haiwezi kuamini? Kwa nini ulimwengu hauwezi kuamini? Haya hapa Maandiko yanayosema inapaswa kuwa hapa wakati huu, nayo hii hapa pamoja nasi.

141 Mwajua, nahofia kanisa limeikokota nafsi yao kupitia kwenye maskini majarida mengi mno ya hadithi ya mapenzi badala ya Neno la Mungu. Hiyo ndiyo shida. Wanaweza kukwambia mengi zaidi kuhusu ni nani mchezaji maarufu wa sinema anayefuata, kuliko kukwambia juu ya matendo ya Roho Mtakatifu. Amina. Hiyo ni kweli. Kama tungaliweka wakati mwingi zaidi wa kukaa Jumanne usiku na Jumatano usiku, na kwenda kanisani kwenye mkutano wa maombi, badala ya kukaa nyumbani tukiangalia televisheni juu ya "Ni Nani Ampendaye Suzie" ama kitu kama hicho, na kukaa mbali na kanisa, tungejua mengi zaidi kuhusu Biblia yetu na kujua yale tunayopaswa kuwa nayo katika siku hii. Kweli. Hiyo ni kweli. Lakini, unaona, sisi—sisi, tumeenda mbali. Mungu ametupa makanisa na—na wachungaji wazuri, na watu waliojazwa na Roho. Na—nasi tunaninii tu. . . Tulizichanganya sana nafsi zetu, tukanenepa na kulishwa, mpaka hatulijali Hilo tena. Loo, jamani! Tunahitaji ku—tunahitaji kutikiswa. Tunahitaji jambo fulani litendeke kwetu. Vema, labda tuliona aibu.

142 Sasa, mimi nilikuja kwenye watu hawa wa Kipentekoste kidogo nimechelewa. Mimi ni mtu aliyezaliwa nje ya wakati wake. Bali ninakumbuka nikisoma historia yake, ule Mtaa wa Azusa. Basi kumbukeni wakati walipokuwa wakifanya

mikutano hii mikubwa, wangeomba usiku kucha. Nao baba zenu, wa—wale wa kale katika kazi, nao wangeomba usiku kucha. Nao wangefunga kwa siku kadhaa, na wangemngojea Mungu mpaka Mungu alipojibu. Leo hii, hatuwezi kukaa madhabahuni dakika tano. Kuna kasoro. Kuna shida gani?

143 Nilikuwa ni—nikizunguka na maskini Mmethodisti wa mzunguko, yeye angeniimbia wimbo mdogo:

> Tuliachilia fito, tuliachilia fito,
> Tulipatana na dhambi.
> Tuliachilia fito, kondoo wakatoka,
> Lakini mbuzi waliingiaje?

144 Tuliachilia fito. Hilo ndilo lililotendeka. Tulipatana. Basi i—inatupasa kuliondokea hilo, ule mkutano wa kale wa Mtaa wa Azusa, ile dini ya kipentekoste, ya mtindo wa kale, ya nyuma ya misitu, anga ya samawati, dini iliyonyoka kama mtutu wa bunduki, inayoua dhambi. Ndugu, hao hawakuipaka chokaa. Iliosha ikawa nyeupe. Iliwafanyia hao watu jambo fulani. Na, leo hii, tulipoyaondokea hayo, tunakuwa walegevu. Tunakuwa kama walimwengu wengine. Ni vibaya mno.

145 Na, leo hii, karibu watu wote hawataki mtu atakayesimama na kuwaambia Ukweli wake. Wanataka maskini Riki fulani aliyekata nywele mtindo wa Hollywood, na amejaa manukato, na kutembea moja kwa moja hapa juu na kuzungumza juu ya theolojia fulani aliyojifunza kwenye makaburi fulani, ama—ama seminari. Samahani. Pote ni mahali pamoja, mahali pa maiti, kwa hiyo basi tu—tunaona hayo kila mahali. Wanataka kitu kama hicho. Hawaitaki Injili ya mtindo wa kale inayotolewa katika nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu tena. Kuna kasoro fulani.

146 Tunahitaji mkutano wa ushuhuda, jambo kuu litukie. Tunahitaji mkutano wa maombi. Tunahitaji kuchimbuliwa, kuraruliwa. Ni kweli. Tunahitaji Kristo arudi miongoni mwetu, kuijua Biblia. Tunaelea tu tukilegea na kulegea, wakati wote. Tunahitaji kurudi kwenye msingi asilia, turudi mahali hapo, ule mwamba tulimotolewa, na kuanza upya tena.

147 Sasa, maskini mwanamke huyu mdogo, alijua mahali alipokuwa amesimama. Hakuna kitu kilichokuwa kinaenda kumkomesha. Naam, bwana. Alikuwa na ushuhuda. Alikuwa ameiona, naye alikuwa akiitazamia. Naye aliyafahamu Maandiko, na alijua hiyo ilikuwa ndiyo. Na mara tu ilipotukia, ikamulika njiani mwake, macho yake yalifumbuliwa, naye akaijua. Hakuna kitu kitakachomkomesha. Kama ni mapokeo ama chochote kile, hakitamkomesha. Kweli. Atalisema, kwa vyovyote vile.

148 Loo, jamani, kwa ajili ya watu kama hao! Tupe nusu dazani wanaowaka moto namna hiyo, ninawaambieni, Tucson patakuwa ni mahali tofauti katika siku chache. Kila mmoja

wenu anataka hiyo katika kusanyiko lenu, sivyo? Sivyo? Naam, bwana. Loo, jamani! Hakika, hilo ndilo tunalotaka, mtu fulani anayewaka moto. Kidogo tulilionea aibu, kwa njia fulani. Tumefikia mahali, tunayaondokea tu Maisha ya mtindo wa kale, yaliyojazwa na Roho ambayo kweli yalitudumisha tukiwa safi.

149 Sasa, Andrea akaanza kutoa ushuhuda. Muda si muda mwajua, ule mtumbwi ukaanza kusukasuka tena. Bali wakaja kugundua, wakati huu, mwajua, jua lilikuwa limetua.

150 Mwajua, na wakati jua linapotua, ndio wakati ambapo uovu huanza, kwa namna fulani. Nilikuwa nikisoma makala fulani katika, ninaamini lilikuwa, jarida la *Life* ama kitu fulani, sio muda mrefu uliopita. Basi mchezaji fulani maarufu wa sinema alitoa tamshi kama hili, "Usiku ulifanywa wa kuishia. Maisha huanza jua linapotua." Mauti huanza hapo jua linapotua. Hapo ndipo pepo wanapozungukazunguka. Waangalie mijusi, nyoka, nge, mende, kila kitu kingine. Hawana budi kuingia gizani. Ni katika giza.

151 Ninyi si wa giza. Ninyi ni wa Nuru. "Tembeeni katika nuru."

152 Inanikumbusha, unaweza kuchukua maskini kiini cha kale cha tofaa, ukiweke sakafuni. Hakuna kitu kitanachokisumbua wakati wa mchana. Acha ifike usiku, na ndipo mende, kila kitu mahali hapo, kitatambaa kwake. Halafu basi kama unataka kuwaona wakitawanyika, washa tu taa. Hakika wanatawanyika.

153 Hiyo inanikumbusha, kama vile kuhubiri Injili. Washa tu Taa. Haichukui muda mrefu sana mpaka uovu uanze kutawanyika. Kanisa linahitaji uamsho mzuri, uamsho mzuri sana wa Roho Mtakatifu, uliotumwa na Mungu.

154 Nilipokuwa mvulana mdogo, mimi na kaka yangu; yule ambaye ameaga; tulikuwa huko nje kwenye kijito siku moja, kilichopitia nyuma ya mahali hapo, nasi tukaona maskini kasa. Sijui kama mnamjua kasa ni, kobe. Wana ganda, mwajua. Nje ni ganda, na kasa ndani. Nasi tukamwona akitembea, na jinsi alivyotembea kwa namna ya kuchekesha. Basi tulipomfikia, alienda "Shh," akarudi kwenye ninii yake . . .

155 Kama tu wengi wa wanaojiita waaminio unapowaambia juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ama kitu fulani. "Loo, hizo siku zimepita." Shh, "Hakuna kitu kama hicho."

156 Jamaa aliniambia, hivi majuzi, kasema, "Sijali unayotoa." Kasema, "Sijali ni watu wangapi waliokufa unaoweza kuthibitisha walifufuliwa, ni wangapi, siamini hilo."

157 Nami nikasema, "La hasha. Haikuwa kwa ajili ya wasioamini. Ilikuwa tu ni kwa ajili ya waaminio. Unaona? Wewe ni asiyeamini." Unaona?

158 Sasa, tulitaka kumwona akitembea, kwa sababu tulifikiri ilionekana ya kuchekesha kuona jinsi alivyoitupa miguu yake. Kwa hiyo nikasema, "Simile. Ondoka." Yeye alikaa tu kwenye

ganda lake. "Vema," nikasema, "Nitamtengeneza, ndugu." Basi nikaenda nikachukua ufito. Nikamcharaza kwelikweli. Huwezi kumcharaza akatoka humo. Alikaa mle tu.

159 Ndipo nikasema, "Mbona, ni—nitakwambia nitakalofanya. Nitamfanya atembee." Basi nikampeleka kwenye kijito. Nikasema, "Nitaninii . . . Ama atatembea, au nita—nita—nitamzamisha." Kwa hiyo nikamtumbukiza majini, na kumshikilia kwa mikono yangu. Basi ni mapovu machache tu yaliyotokea, naye akakaa kwenye ganda.

160 Ubatizo wa maji hautoshi, ndugu. Unaweza kuwabatiza vyovyote utakavyo. Hilo halitoshi. La, la. Hiyo ni kweli. Huenda ukapata mapovu machache, lakini karibu hayo ndiyo yote.

161 Ndipo nikaona kipande cha karatasi kilichokuwa hapo pembeni. Nikajiwashia moto kidogo, kisha nikamweka juu ya huo. Ndugu, alitembea wakati huo.

162 Hilo ndilo kanisa linalohitaji usiku wa leo, linahitaji Roho Mtakatifu na Moto, kulifanya kanisa lisonge kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Litasonga basi. Uamsho, kumkubali Kristo, Neno! Liamini Hilo, acha Hilo lizame chini ya ubavu wa tano kwenye mkono wa kushoto, mpaka Hilo litie nanga, sehemu ya chini ya moyo. Halafu, mafuriko ya furaha yatabubujika, na furaha isiyoneneka, na iliyojaa utukufu. Naye Roho Mtakatifu atawafanya muimbe, "Yajaze mapito yangu kila siku kwa upendo, ninapotembea na Hua wa Mbinguni." Itakufanyia jambo fulani. Kile tunachohitaji, ita—itaweka nguvu mle ndani. Itakufanyia jambo fulani.

163 Kwenye wakati huo, ndugu hawa, jua likatua, giza likaanza kuingia. Hapana shaka Shetani alikuja kutoka kwenye mashimo yake ya mateso na kuangalia huko juu ya kilima. "Aa!" Ilimbidi akae kimya siku hiyo, kwa sababu mambo makuu yalikuwa yakitukia. Kwa hiyo yeye . . . Giza likaingia, naye akaangalia juu ya kilima. Nao wanafunzi walikuwa wameondoka bila Yesu. Hilo tu ndilo alilotaka. Aliwakuta bila Yesu.

164 Na hapo ndipo tu anapotaka kukushikia. Hamuamini ya kwamba kukata nywele zenu ni kosa, enyi wanawake. Hebu rudini tu kwenye Biblia na muone kama ni sahihi ama si sahihi. Hamfikiri mambo haya ni mabaya. Yeye anawashika mkiwa mbali na Yesu. Hivyo tu. Hebu ishi maisha mazuri, ya kitauwa, na uone kinachotukia. Watu wengine wanasema . . .

165 Mwanamke aliniambia, hivi majuzi, alisema, "Ndugu Branham. Ninataka kukwambia sasa hivi. Ulikuwa ukizungumza juu ya magauni yetu, jinsi tulivyokuwa tukiyavalia, yamebana sana ngozi iko upande wa nje."

Nami nikasema, "Vema, ninataka kukwambia jambo fulani."

Akasema, "Hiyo ndiyo aina pekee ya gauni wanaloshona sasa."

166 Nikasema, "Huo si udhuru. Wangali wana vitambaa na wana cherahani. Huwezi kupata. . .Hakuna udhuru kwa ajili yake, hata kidogo. La, bwana." Nikasema, "Endelea, na siku moja utajibu kwa kufanya uzinzi."

167 Sijali jinsi ulivyo safi, jinsi ulivyo safi kwa mumeo, mpenzi wako mvulana. Ukijivika kwa kuvutia kimapenzi kabisa na kushuka kwenda barabarani, mwenye dhambi fulani akuangalie kwa njia mbaya, basi kwenye Siku ya Hukumu, yeye ataliwajibikia jambo hilo. Na ni nani aliyelifanya? Wewe. Yesu alisema, "Yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Na wewe ulijianika namna hiyo.

168 Mungu, tutumie uamsho kabla hatujaangamia. Hiyo ni kweli. Tunahitaji uamsho wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu, unaochochea nafsi, naam, tumwone Kristo amerudi miongoni mwetu, tumwone Kristo katika madhabahu ya mtindo wa kale na mikutano tuliyozoea kuwa nayo miaka kadhaa iliyopita.

169 Sasa, Shetani alisema, "Wameondoka bila Yeye, nami nimewapata mbali. Nafikiri. . . "

170 Hivi huamini, ndugu, sasa? Tunajua kuna madhehebu yote mbalimbali hapa, na—nami ni mfuasi wa yote. Kwa hiyo, lakini, msije mkafikiri ya kwamba wakati huu wa ufanisi. . .Tumekuwa tukijenga mijengo mipya. Tumekuwa tukinunua kila kitu kipya, na kusanyiko lote lina pesa nyingi, na wanavalia vizuri zaidi. Nafikiri kwa namna fulani tulienda kombo kwa namna fulani ya hamaki, nasi tumemwacha Kristo mahali fulani. Mnaona?

Na sasa yeye anatuona tumeketi hivi hapa nje.

171 Uamsho umekwisha. Na sisi hapa, sio muda mrefu uliopita, mbona, uamsho ulikuwa ukiwaka moto, na sasa inaonekana kwa namna fulani ni vigumu kulijaza kanisa. Wachungaji wananiambia kwamba ni—ni vigumu, siku hizi. Nao watu hawataenda kanisani. Afadhali wakae nyumbani na kuangalia televisheni, na, ama kitu fulani. Upendo umeondoka moyoni mwao.

172 Naye Shetani ametuona tukienda kombo kwa hamaki hii, na kuondoka bila Yesu, naye anafikiri ndiyo nafasi yake.

173 Kasema, "Sasa nitawazamisha. Wakati nikiwapata wameondoka, nitawazamisha. Hilo ndilo jambo tu nitakalofanya. Nimewashika sasa bila Kristo. Walimwacha Yeye nyuma."

174 Na, mnaona, walikuwa na shughuli nyingi sana, na walikuwa na mengi ya kufanya, huku wakiwapungia watu mikono, na mambo mengi sana ya jamii, na kila kitu, hata wakasahau kumchukua Yeye pamoja nao.

175 Nafikiri hilo ndilo tumepata, mipango yetu mingi kupita kiasi, hata tumemwacha Yesu nje. Mambo ambayo baba na mama yetu waliyapigania sana, wakalala kwenye njia za reli, na kula mahindi, na ngano, na chochote walichoweza kupata, wapate kuihubiri Injili hii. Na leo hii tunagaagaa tu matopeni. Mnaona? Sio sahihi. Inatupasa tuwe tunawaka moto.

176 Basi Shetani anaona hili, naye ni kama tu ilivyokuwa wakati huo. Akasema, "Nitawazamisha huko nje, usiku wa leo, kwa sababu Yesu yuko mbali nao." Sasa, upepo ukaanza kuvuma. Shida ikaanza kuingia. Na ilionekana kana kwamba hakuna mtu aliyekuwa na jibu.

177 Sasa tunayo makombora ya haidrojeni na wanaanga, na kila kitu kingine, lakini inaonekana kana kwamba hakuna mtu aliye na jibu. Wanafanya kila namna ya makongamano na mikutano, wakijaribu kuona kama hawawezi kumshinda mtu fulani kwenda mwezini. Sina wasiwasi kuhusu kufika mwezini. Ninataka kwenda zaidi ya mwezi, nitakapoanza kwenda juu.

178 Nao wamepiga mayowe hapa, Urusi ilipiga, sio muda mrefu uliopita, kuhusu kuwa na mtu angani, walikuwa na mtu wa kwanza angani. Loo, jinsi walivyo nyuma kwa mbali! Tumekuwa na Mtu angani kwa muda wa miaka elfu mbili. Jamani! Utukufu! Tunapaa juu pamoja na Yeye, baadhi ya siku hizi, Yeye. Hakika!

179 Lakini, mnaona, ni kitu kama, vita vya hadhi. Nao hapa wakaanza kupiga makelele, ndipo Shetani akaanza kupuliza maskini pumzi lake lenye sumu juu yao, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Yuko wapi Bwana wenu sasa? Huyu hapa mtu fulani katika kusanyiko lenu, aliye mgonjwa, na inaonekana kana kwamba hamwezi kuwafanyia lolote." Mnaona, ni kazi bure tu. Mnajua nini? Walikuwa na mkutano hivi majuzi, nasi tunasikia ya kwamba watachukua, kwenye kumbukumbu zetu ama kanisani mwetu, wanaenda, wanaenda kufutilia mbali uponyaji wa Kiungu. Makanisa mengi yanafanya hivyo, hawauamini tena. Wachungaji wengi hawauamini.

180 Jinsi mlivyo na bahati nyinyi watu kuwa na wachungaji wa kipentekoste ambao watatetea jambo ambalo Kristo alitetea.

181 Moja ya madhehebu yetu makubwa ya Kipentekoste hivi majuzi tu lilitoa taarifa, kwamba, kabla hawajaweza kuwatuma wamishenari wao nje, inawabidi kwenda mbele za mtaalamu wa magonjwa ya akili, waone kama IQ zao ni za juu vya kutosha. Loo, kama hiyo si Pentekoste!

182 Sijui ni kiasi gani cha elimu Petro angekuwa nacho kama wangalimpima huko? Hiyo haikuwa . . . Hilo hata halikuwaziwa. Haikuwa kwamba walikuwa na IQ kiasi gani. Ni kiasi gani cha nguvu za Roho Mtakatifu walichokuwa nacho, kudhihirisha nguvu hizo, ni aina gani ya maisha waliyokuwa wanaishi. Hakika.

Sasa, tunaona ya kwamba upepo wa sumu umeanza kuvuma. Umekipeleka maskini chombo hicho kwenye kitu kingine.

183 Na sasa kumbukeni, mimi ninathamini yote Mungu anayotufanyia. Ninathamini kwamba tuna magari mapya. Ninathamini kwamba tumetoka kwenye—tumetoka kwenye matambara, tukaingia kwenye nguo nzuri. Ninathamini hilo. Lakini, mnaona, tunapoanza kupata vitu hivyo . . . Tuna makanisa makubwa mashuhuri.

184 Ilikuwa kwamba, baba zenu, baba zetu, baba zetu wa mwanzoni, walisimama hapa nje mtaani, kisha wakalala usiku kucha gerezani, kwa sababu ya kufanya mkutano wa ushuhuda. Walikuwa na maskini ghala dogo huko chini, ambalo wadudu karibu walikuwa wameliangamiza, katika tundu lililojaa panya. Walimwacha alichukue kwa dola mbili kwa juma. Ndipo angeshuka aende kule, aanze, kisha liwali angelishika kundi hilo lote kabla ya usiku kwisha. Hivyo ndivyo ilivyowabidi kuipiga vita.

185 Na sasa tuna makanisa yaliyo makubwa kuliko yote mjini, umati uliovalia nadhifu kuliko wote, na kila mtu mwingine akija. Lakini ziko wapi zile nguvu za mtindo wa kale, za Roho Mtakatifu zilizotumwa na Mungu, walizokuwa nazo kule nyuma? Kasoro fulani mahali fulani. Mahali fulani, kuna kasoro. Tunaishi kupita kiasi . . . Sisi ni wororo kupita kiasi.

186 Mwanadamu anakuwa mwororo. Wanakuwa machotara. Hiyo ni kweli. Hebu chukua miaka hamsini iliyopita, m—mchezo wa besiboli, kamwe hukusikia kuhusu ajali. Sasa wanawaua dazani moja kwa mwaka. Ukimgonga mmoja, yeye ni kama tu kanga, inammaliza, amekufa.

187 Mwangalie Bob Fitzsimmons, na—na Corbett, John L. Sullivan, na hao watu waliopigana kadiri ya raundi mia moja na ishirini na tano katika alasiri moja. Na raundi moja haikuwa dakika mbili au tatu, ilikuwa ni kubwaga chini. Kuangushana, mara ishirini na tano katika alasiri moja, kote. Hawakuwa na glavu za manyoya mikononi mwao kama wanandondi walivyo nazo siku hizi. Walikuwa mikono mitupu. Wangechukua konde la nchi nne na kupasua mbili-kwa-nne kwa mikono yao. Wangeweza kustahimili hiyo. Walikuwa ni wanaume.

188 Na sasa maskini hawa akina riki, wanavyojiita, waliolishwa kwa vitamini, wamevaa glavu za manyoya. Nao wamefikia, itawabidi kukomesha kitu hicho chote cha ndondi. Imekuwa wororo. Mwanadamu amekuwa mwororo. Hamna kitu ndani yake tena. Yeye ni kitu kikubwa mno kinachoonekana kama jitu, bali ni kitu gani? Lundo la shahamu. Vile tu hasa Biblia ilivyosema, "Wanakuwa wanyonge zaidi bali wenye hekima zaidi." Ni kweli. Machotara!

189 Kitu chochote ninachokidharau ni chotara. Nimeona makala kwenye Readers Digest. Wakiendelea kuwalisha wanawake na

kadhalika, chakula hiki chotara, kwamba katika miaka ishirini tangu sasa kizazi chote cha watu kitaangamia. Wanawake wanakuwa wapana mabegani, nyonga nyembamba. Hawawezi kuzaa watoto wao na kadhalika. Machotara!

190 Nena kuhusu mahindi chotara. Hakuna kitu ndani yake. Ni kitu gani? Punje kubwa mno nzuri, bali hakuna kitu ndani yake. Hebu chukua hayo mahindi chotara ukayapande tena, hupati chochote. Yamekwisha, kuchanganya kitu chochote.

191 Na hivyo ndivyo kanisa limekuwa hasa, lundo la machotara. Ni kweli. Wameuchanganya ubatizo wa Roho Mtakatifu na kujiunga na kanisa, nao wamepata kundi la wanaokiri kuwa Wakristo, wanavyojiita, wenye miguu miororo, ambao hawajui zaidi kumhusu Mungu kuliko sungura anavyojua kuhusu viatu vya theluji. Mnajua hiyo ni kweli. Tunachohitaji leo hii ni ujuzi wa Biblia utakaorudisha kwa kuzaliwa upya, uliotumwa na Mungu. Chotara! Wanasema inaonekana nzuri zaidi. Hicho ndicho walicho nacho. Tuna majengo makubwa zaidi, makutano yaliyovalia vizuri zaidi. Bali tuna nini? Tuna punje kubwa ya mahindi, bali hakuna uhai ndani yake. Tuna kanisa kubwa zaidi na tabaka la watu lililoelimika vizuri zaidi, lakini uko wapi Uhai? Hawawezi kujizaa wenyewe tena.

192 Kama nyumbu. Daima nilimhurumia nyumbu. Nyumbu hata hajui. . .Hana ukoo safi. Mama yake alikuwa farasi jike, na baba yake alikuwa punda. Hata hawezi kupata watoto, yeye mwenyewe. Hawawezi kuwazalisha, tena. Huwezi kuwazalisha tena.

193 Hilo liliibwaga sayansi chini, kasema, mabadiliko yanayoendelea yalisema ya kwamba tulitoka kwenye tumbili. Tungewezaje? Unapomzalisha wakati mmoja, hawezi kuzalishwa tena. Hilo linaibwaga chini hoja yao. Hiyo ni kweli. Haiwezi.

194 Angalieni. Naye maskini nyumbu huyu, hajui. Hajui. Hajui chochote. Na yote ajuayo, yeye ni nyumbu tu. Sikuzote yeye huangalia. . .Anaketi hapo na masikio yake makubwa yaliyosimama, mwajua. Nawe ukianza kuzungumza na yeye, huwezi kumfunza chochote. Huwezi kumfundisha kitu. Anakukazia macho tu, anaanza, "Hoo! Hoo!" Hivyo tu ndivyo anavyofanya.

195 Inanikumbusha juu ya kundi la watu walioketi pale kama baadhi ya hawa nyumbu, dini chotara tuliyo nayo. "Siku za miujiza zimepita. Hoo! Hoo! Hoo!" Anajua nini kuzihusu? Hiyo ni kweli. Hajui. Hajui baba yake alikuwa nani. Jambo pekee ajualo, wao ni wafuasi wa dhehebu fulani.

196 Lakini ninapenda farasi halisi wa ukoo safi, ukoo safi. Anajua baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani, babu wa baba yake, nyanya wa mama yake. Anajua walikuwa akina nani, maana yeye ni ukoo safi.

197 Nami ninampenda Mkristo halisi mwenye ukoo safi. Anajua anakotoka, kwa ajili ya ubatizo asilia wa Roho Mtakatifu kwenye Siku ya Pentekoste. Utukufu kwa Mungu! Yeye ni ukoo safi na ametiwa muhuri na Ufalme wa Mungu.

198 Ukisema, hivi Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Maskini nyumbu huyo atapiga makelele, "Loo, kwa njia fulani, kwa njia fulani."

199 Lakini wa ukoo safi atasema, "Amina." . . .?. . . Unaamini katika uponyaji wa Kiungu? "Amina." Ujuzi halisi wa Mungu utaitikia kila ahadi kwa "amina." Utukufu!

200 Sikukusudia kufanya hivyo. Hebu tuanze nyuma. Nilikuwa wapi? Kwenye mkutano wa ushuhuda. Angalieni. Nitayaacha hayo kwa wachungaji wenu. Vema.

201 Angalieni, dhoruba kubwa ikaanza kutokea. Shaka likaanza kuingia. Msukosuko ukaanza kuingia. Hivyo ndivyo ilivyotendeka, mnaona, uchotara unarudi tena. Mnajua nini? Mmea halisi asilia, haikubidi kuunyunyizia. La, bwana. Wadudu hata hawatauendea. Ni mmea wa kibanda cha kuoteshea ndio unaokulazimu kunyunyizia.

202 Hiyo ndiyo shida. Inakubidi kunyunyizia, na kubembeleza, na kudekeza wale wanaojiita Wakristo. Ukiwaambia, hamwezi kufanya *hivi*. "Loo, vema, sasa, nitakwambia tu, ninayo haki." Haya basi. Mnaona? Huo ni mmea wa kibanda cha kuoteshea. Hawawezi kuvumilia chochote, tangu mwanzo, mnaona. Unachohitaji ni kuchimbuliwa asili, mtindo wa kale, na kuraruliwa kabisa. Na kama nilivyosema jana usiku, safisha kiota na uanze upya. Hiyo ni kweli. Unaweza kuwafanya mashemasi na kila kitu kingine, bali halitafaa kitu. Uwapapase mgongoni na kuwaita ndugu, lakini, mpaka watakapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, hao ni kiota tu kilichojaa mayai yaliyooza. Hivyo tu. Kamwe hayataanguliwa. Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Simaanishi kupeana mikono kukavu.

Na kusema, "Hivi wewe, hivi ulimpokea Roho Mtakatifu?"

203 "Naam, nilipopeana mikono na mchungaji, nilipomkubali Yesu kama Mwokozi wangu." Ndugu, hilo si Fundisho la Biblia.

204 Paulo alikuta kundi la Wabaptisti ukoo safi huko juu, naye akasema, "Mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?" Si *wakati* mlipoamini. Bali, "Baada ya kuamini, mmempokea Roho Mtakatifu." Ni ujuzi wa kibinafsi unaokuja. Basi wakati yule Mungu mkuu asiyebadilika alipoushusha Ujumbe Wake, Yeye kamwe habadiliki. Amina.

205 Sasa tunaona kuna shida. Kuna shida gani? Jambo fulani limetukia. Chombo kinasukwasukwa. Upepo unavuma. Shetani anakirusharusha hicho chombo, pigo baada ya pigo, wimbi

baada ya wimbi. Nayo matumaini yote yamekwisha, ya kuwa na uamsho mwingine.

206 Shuhuda zinaisha. Heri wakae nyumbani na kuangalia televisheni. Mnaona? Hakuna tena mikutano ya Jumatano usiku ya ushuhuda na kadhalika, hakuna tena mkutano wa maombi. Mnaona?

207 Makasia yalivunjika. Mlingoti ukaanguka, usukani. Yote yamekwisha. Upepo wote tayari umeangusha matanga yote.

208 Na masumbuko ya ulimwengu hivi karibuni yatauangamiza ushuhuda wote kutoka kwako, pia. Unaona aibu kuamka. Kwa nini? Unajua. Unajua kile unachoishi. Unajua huishi kulingana na hilo. Basi, nawaambieni, tunachohitaji ni uamsho.

209 Hao hapo, kama tu tulivyo leo hii. Lakini mnajua nini? Hakuwa kweli amewaacha. Mwajua, Biblia ilisema ya kwamba Yeye alikuwa amepanda moja ya vilima virefu sana vilivyokuwamo nchini, kusudi aweze kuwaangalia. Na hivyo ndivyo alivyofanya wakati alipotuacha pale Kalvari. Yeye—Yeye—Yeye . . . Wakati walipomsulubisha, Yeye kamwe hakutuacha. Hakupanda kilima kilicho kirefu kuliko vyote, bali alipanda Kalvari, na akaendelea kupanda kupita mwezi, nyota, kuendelea hata kuingia katika mbingu za mbingu. Kadiri unavyozidi kwenda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali. "Basi Yeye alifika juu sana, hata inambidi kuangalia chini aione Mbingu," Biblia inasema. Naam. "Alikuwa juu sana kwenye mbingu za mbingu, akapaa Juu."

210 Jicho lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye anatuangalia usiku wa leo. Hiyo ni kweli. Yeye anaangalia chini kwenye mkutano huu. Anaona shida yetu. Anajua masumbuko yetu. Anajua jinsi ulivyo mgonjwa. Anajua yale uliyopitia. Anajua yale unayojaribu kufanya. Mnaona? Jicho Lake linakuangalia.

211 Naye alikuwa amesimama juu ya ule mlima, akiangalia, akiangalia. Akaona shida yao. Aliona makasia yakivunjika. Aliona kusanyiko likiondoka, tuseme. Aliona kila kitu kikitendeka. Aliona Shetani akianza kuwapulizia kote, akiwanyonganyonga huku na huku, kwa kila njia, ambapo hata hawajui la kufanya. Basi kulifanyika nini? Wakati matumaini yote yamekwisha, kwamba kamwe wangeweza, kamwe wangeweza kuokolewa, kulifanyika nini? Ndipo walipomwona akija akitembea juu ya maji. Akaja kwao akitembea.

212 Sasa, kama angalikuwa kwenye hicho chombo, pamoja nao, kisha aondoke akitembea, wangalilikubali. Lakini, mnaona, Yeye alikuwa mbali nao, na ilimbidi kuja akitembea, juu ya maji. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Waliogopa. Walishtuka." Wakasema, "Ni kivuli." Na kitu pekee ambacho kingaliweza

kuwaokoa, walikiogopa kwa sababu kilionekana kama mzuka. Walikiogopa.

213 Kama hiyo si picha ya leo hii, kamwe sikuisimulia. Kitu pekee kinachoweza kuwaokoa watu, wanakiogopa Hicho: Yesu Kristo. Katika majira haya ya msiba tuliyomo, wakati kanisa likiwa karibu tu kuingia kwenye muungano wa makanisa, na kwenye Baraza la Makanisa Ulimwenguni, na—na mambo haya yote, na madhehebu yetu yanakuja, yamekaushwa kabisa, na kila moja. Nanyi mwajua. Sote tunajua hilo.

214 Wabaptisti wetu na Wapentekoste wetu, wakienda njia ile ile. Tunawapenda ndugu zetu, na kila mahali, haijalishi mahali walipo. Lakini kamwe dhehebu halikuwahi kujiundia dhehebu, likaanguka, ambalo lilipata kuinuka tena. Sasa, hebu ichunguze tu historia. Wanapoondoka, wamekwisha. Na madhehebu yetu ya Kipentekoste! Sasa, mfumo huo, sio ndugu, bali mfumo wa kimadhehebu umekwisha. Linapata tu joto. Linaninii tu. . . Limekuwa vuguvugu, na linakuwa tu baridi kama barafu. Mnaona, li—linaondoka. Nao watu wanaingia baridi, na wa kawaida, na kuyashughulikia mambo ya ulimwengu. Nasi tunapata kila kitu kizuri na kikubwa, mwajua, na tunakabidhiwa tu kila kitu mkononi mwetu.

215 Mungu aliwaambia Israeli, "Ulipokuwa huna kitu, nilikupata kondeni umelowa damu na nikakuosha." Alimthamini Mungu. Bali ulipokuwa mkubwa, na ukaanza kupata mali nyingi, basi walimsahau Mungu.

216 Na hivyo ndivyo tu limeanza kuwa. Mnaona? Na sasa, mnaona, wakati mambo yote yanaonekana kuwa kwamba ninii yetu. . . Tumeanza kuangalia huku na huku, "Ni washiriki wangapi zaidi tunaoweza kupata? Ni kusanyiko kubwa zaidi jinsi gani? Tunaweza kupata kanisa kubwa kidogo zaidi kuliko ndugu huyu mwingine upande ule mwingine wa mji? Tunaweza kuwa na mbio ngapi za shule ya Jumapili?" Na kuwapa pini ya dhahabu kwa kufanya jambo fulani, kuwaleta wengi *sana* kwenye shule ya Jumapili. Wabaptisti walikuwa na msemo mdogo pale, hata hivyo, katika '44, kasema, "Milioni moja zaidi katika '44," wito. Mlipata nini mlipoingia mle?

217 Tukiketi na Billy Graham, si muda mrefu uliopita, aliweka ninii yake. . . alisimama pale, na kuinua Biblia juu. Akasema, "Huu ni Mfano wa Mungu." Nilikuwa kwenye kiamshakinywa chake. Akasema, "Mimi. . . Mtakatifu Paulo alilichukua Neno hili la Mungu, kisha akaingia mjini, na kuhubiri, na akampata mwongofu mmoja. Alirudi mwaka mmoja baadaye, naye alikuwa na theluthi moja. . . thelathini kutoka kwa huyo mmoja. Huyo mwongofu mmoja aliwaongoa thelathini." Naye akasema, "Yeye alikuwa na wajukuu thelathini basi, mnaona, kutoka kwa mtoto huyo mmoja." Akasema, "Ninaingia mjini, nitakuwa na maungamo elfu thelathini. Ndipo ninarudi katika mwaka

mmoja, siwezi kupata thelathini." Basi akasema, "Sasa, kuna shida gani?"

218 Ninamthamini mwinjilisti huyo. Nafikiri Mungu anamtumia huko nje katika hiyo, mahali alipo. Inapasa pawepo mtu wa kwenda Sodoma, mwajua. Wote hawawezi kudumu pamoja na Ibrahimu na kundi lake, waliovutwa wakatoka, Wateule. Bali kulikuwako na mmoja aliyekaa kule, akaonyesha ishara fulani, akawaanda kwa ajili ya kuondoka. Angalieni.

219 Ndipo Billy akasema, "Mnajua shida ni nini?" Hakuwachezea. Alisema, "Ni ninyi kundi la wahubiri wazembe," akasema. Akasema, "Nitawapa kadi hizi za kukata kauli, nanyi mtaketi huko nje, na kuweka miguu yenu juu ya dawati, na hata hamtaenda kuwasumbua; na—na labda muwaandikie barua, na kuwaambia mngetaka kuwachukua, mshiriki wa kanisa lako. Mnapaswa kutoka huko nje na kuwashawishi, na kuwaleta kanisani."

220 Vema, niliketi na kuangalia, kwa kitambo, mwajua. Nikawaza, "Hilo linasikika zuri sana." Nikawaza, "Loo, Ndugu Graham. Kwa hakika ningetaka tu kukuuliza swali sasa hivi. Lakini mimi ni maskini mtu duni tu, unajua, na wewe ni mtu mashuhuri. Kwa hiyo ni—nisingefanya hivyo. Lakini ningetaka kusema, 'Ndugu Graham...'" Jambo ndilo hili, kama ningalimwuliza.

221 Sasa, kumbukeni, si kumshutumu, maana ninampenda. Na yeye ni mtu mashuhuri. Ninamwombea, wakati wote, nasi hatuna budi kufanya hivyo.

222 Na sasa, ningetaka kusema, "Ndugu Graham, ni nani, alifanya nini jamaa huyu, akiwa na huyu mwongofu mmoja ambaye aliletwa na Paulo, ni mhubiri gani alichukua, akaenda kwake?" Maana, hakuwa na mchungaji wa kuachwa naye. Mnaona?

223 Kulikuwa na shida gani? Paulo hakuachia tu kwenye maungamo. Alidumu pamoja naye mpaka akapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Alikuwa anawaka moto, na karibu aunguze mji mzima. Hiyo ndiyo shida.

224 Hiyo ndiyo shida leo hii. Tunawaingiza tu kama maungamo, badala ya kuwapeleka mbele wakampokee Kristo, mpaka wamezaliwa kwa Roho wa Mungu. Hiyo ndiyo tunayohitaji leo hii, ni hiyo mikutano ya usiku kucha. Sio tu kukaa... Ninaamini katika mambo yetu yote tufanyayo. Ninaamini katika kupaza sauti; ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini katika kufasiriwa kwa lugha. Ninaamini katika uponyaji wa Kiungu. Ninaamini katika mambo hayo yote. Lakini, hata hivyo, ni kitu fulani bora zaidi ya hicho. Ni Kuzaliwa, kwenyewe. Ni Roho Mtakatifu, Mwenyewe, akiingia ndani yetu. Mambo haya ni mazuri. Lakini wewe... Hilo ni jema. Lakini, ni kama yule mtu mweusi akila tikiti maji, "Kuna zaidi." Inakubidi kuendelea,

mpaka upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, subira, nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo zichome kuingia ndani ya maisha, ndipo tungeweza kuwa na mkutano wa ushuhuda juu ya yale Mungu anafanya miongoni mwetu. Hiyo ni kweli.

225 Yesu alikuja kwao akitembea, juu ya maji, nao wakaogopa. Wakasema, “Loo, ni—ni—ni kivuli. Sisi, heri tusiende kwenye mkutano huo tena. Ni wa kigeni.”

226 Walimwona akirudi tena, katika nguvu Zake; kama tu Yeye alivyoahidi kupitia kurasa za Biblia hizi, kwenye kurasa hizi—hizi katika Biblia hii, hasa, kwamba Yeye angefanya jambo hili katika siku za mwisho. Nazo zinaingia, na wengi wa watu wanasema, “Aah, Huko ni kuwasiliana kimawazo tu. Huo ni ushirikina. Hiyo ni namna fulani ya . . . ” Mnaona? Hilo ni jambo lile lile. Na kitu pekee kitakachookoa, kitakachotusaidia tutoke kwenye hili, ni kumkubali Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Angalieni. Wakati Yeye alipokuwa . . .

227 Wote waliogopa, nao wakapiga yowe, “Loo, ni kitu gani Hiki? Hatujui.” Kilionekana cha kutisha. Kilionekana kivuli. Kulifanyika nini?

228 Papo hapo kwenye muda huo muhimu, kukaja Sauti, “Msiogope. Ni Mimi. Msiogope.”

229 Usiku wa leo, kama vile ningesema hili, tunamalizia maskini ushuhuda wetu hapa. Inanibidi kufanya hivyo, upesi. Na ninafunga ushuhuda wao, katika kufunga sehemu hii ya uamsho. Enyi marafiki, mnapomwona Yesu Kristo akifanya jambo fulani kama vile amekuwa akifanya hapa, mkutano wetu wa siku nne usiku ni mfupi sana. Ningetaka kusimama hapa na kuichukua Biblia hii, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo, na kuwathibitishieni kwamba hiyo ndiyo ile saa hasa tunayoishi. Haya yanapaswa kutukia. Kulingana na Biblia, ndiyo saa ya mwisho.

230 Wakati mimi na Billy tulipoenda India kwa ndege, hivi majuzi tu, walikuwa na kipande cha gazeti. Ni nchi ya lugha mbili. Nalo lilisema, “Hapana budi matetemeko ya ardhi yamekwisha. Ndege wanarudi.”

231 Sasa, India, hawana nyua hizi nzuri zilizosokotasokota kama tulizo nazo. Wao huokota mawe na kufanya nyua zao, na kujenga nyumba zao, na wengi wao. Na kwa siku moja ama mbili, maskini ndege wote walioishi kwenye mawe haya waliruka, na kuondoka. Wasingerudi kwenye hayo mawe, kurudi kwenye kiota chao. Ndipo basi kulifanyika nini? Ng’ombe wote waliozoea kuja ji—jioni, wakati jua lingekuwa joto, nao wangesimama kwenye vivuli vya kuta hizi, wapate baridi; kondoo; wasingefanya hivyo. Walienda moja kwa moja katikati ya uwanja na kusimama wameegemeana.

Wakawaza, “Ajabu hii. Wamepatwa na nini?”

232 Ndipo basi, mara ghafla, tetemeko la nchi likatokea kote nchini. Kuta zote zikaanguka. Halafu lilitulia kwa siku mbili au tatu, matetemeko ya nchi. Halafu, kwa ghafla, kile kilichoachwa kimesimama, maskini ndege hao wakaanza kurudi tena, kurudi. Wakasema, "Matetemeko ya nchi hapana shaka yamekwisha."

233 Hivi hamwoni, enyi marafiki? Mungu yeye yule katika siku za Nuhu, ambaye angeweza kuwachukua ndege na wanyama, na kuwaweka katika safina ya usalama, mbali na maangamizi, Mungu yuyo huyo angali anaweza kumwonya ndege. Naye ndege huongozwa tu na silika. Kama ndege, kwa silika, Mungu akimwonya aziondokee hizo kuta kubwa zinazoporomoka, hakika, kwamba kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwamba tunaweza kuziondokea maskini kuta hizi kubwa za kale zikiwa ni mapokeo yaliyojengwa kutuzunguka, na kutoka huko nje, kama ikitubidi kusimama, mmoja akimwegemea mwenzake, na kukaa kwenye kivuli cha Biblia. Hiyo ni kweli. Yeye . . .

234 Msiogope. Yeye aliliahidi. Yeye anakuja akiendesha moja kwa moja kuingia ndani yetu, na kutenda kazi Zake. Na hebu tusiogope, usiku wa leo. Kama tungeweza tu kuifungua mioyo yetu na kusema, "Bwana Yesu!"

235 Angalia nyakati za usiku. Angalia, angalia tu, maskini siku zetu usiku, wakati hatujapata kuwa hapa hapo kabla katika mkutano. Na huu ni usiku wa—wa nne tu. Siku tatu usiku zimepita. Basi angalieni, Roho Mtakatifu hajashindwa hata wakati mmoja. Ninapata barua za shuhuda zikija kutoka mahali mahali, na kusema yale yangetokea walipofika nyumbani, na kadhalika. Walisema ilikuwa ni vivyo hivyo hasa. Mbona, hakika. Daima itakuwa hivyo. Mnaona?

236 Angalieni inachosema. Wakati tu unapoisikia ikinena, angalia inachokwambia. Mnaona? Ninasema basi kile ninachoangalia. Basi ngoja na uone kile Yeye anachokwambia ufanye. Chochote anachokwambia ufanye, nenda, ukifanye. Sijali ni kitu gani. Nenda, ukifanye. Si ndugu yenu hapa; ni Yesu Kristo. Mnaona? Ni Kristo. Yesu alisema wakati alipokuwa hapa, "Si Mimi; ni Baba." Mnaona? Baba alikuwa akitenda kazi kupitia Yeye. Sasa, Baba anafanya kazi kupitia Kanisa Lake, mnaona, Roho Mtakatifu.

237 Nawe unapoliona Hilo, usiliogope Hilo. Likumbatie, useme, "Bwana Yesu, ninakupenda. Wewe upo hapa. Labda sijawahi kukukubali Wewe kama Mwokozi wangu. Usiku wa leo nitafanya hivyo. Ninakutaka Wewe uwe Mwokozi wangu. Sitaki mkutano huu ufungwe mpaka nimeokoka. Ninataka Wewe uniokoe usiku wa leo, Bwana." Atafanya hivyo. Atafanya hivyo. Hiyo inathibitisha tu kwamba Yeye yupo hapa. Tuko katika siku za mwisho. Mambo haya yanapaswa kuwepo.

238 Basi kumbukeni, ishara ya mwisho aliyopewa Ibrahimu, ambaye alikuwa ni mfano wa wale watakaoingia katika

Unyakuo. Mnaona? Walikuwa tayari wametoka Sodoma. Ishara ya mwisho aliyopewa ilikuwa ni ishara hiyo hiyo: Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, ambaye alimwambia Ibrahimu yale Sara alikuwa akiwazia, katika hema nyuma yake. Naye Yesu anageuka moja kwa moja na kusema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu.”

239 Ninachukulia kuwa ninyi watu ni wa kiroho. Tafadhali jaribuni kuelewa. Mnaona? Hii huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Mnaona? Labda hamkufundishwa haya katika makanisa yenu, makanisa yenu mazuri makubwa. Hao watu, sina neno dhidi ya mchungaji wako sasa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “ . . . msiogope. Ni mimi. Msiogope.”

240 Sasa, Baba wa Mbinguni, maskini mkutano huu fidhuli wa ushuhuda, uliokatikakatika niliokuwa nikijaribu kuelezea, na kujaribu kuwaonyesha watu ya kwamba tungeweza kuwa na ushuhuda ule ule katika kila moja ya makanisa haya Jumapili. Makanisa haya mazuri yaliyoketi hapa, ambao ni minara ya taa, kunaweza kuwa na watu wanaosimama mle ndani, Jumapili asubuhi, wakitoa ushuhuda wa jambo lile lile ambalo walikuwa wakishuhudia kulihusu usiku ule baharini. “Loo, mioyo yetu haikuwaka wakati tulipomwona Yeye akifanya *hili*, na tukamwona akifanya *lile*?” Mungu, naomba, tuma uamsho mkuu, Baba. Tushike, Bwana. Tuna—tunahitaji uamsho mkuu. Jifunue Mwenyewe kwetu, kwa njia halisi, usiku wa leo.

241 Labda, Bwana, baada ya mkutano huu wa ushuhuda ambao nimenena habari zake, labda itatokea njaa kubwa sana kwenye mioyo ya watu, kama Wewe utajitangaza tu Mwenyewe tena usiku wa leo miongoni mwa watu. Ndipo wataondoka hapa, na Jumapili asubuhi watayajaza makanisa hayo na kushuhudia. Wataondoka hapa, wawaendee majirani wao, na waanze kuzileta nafsi, na kujaribu, wakipiga magoti pamoja na majirani wao, na kuomba pamoja nao, na kwenda, kutembelea hospitali, wagonjwa na wanaoteseka, na kuwaambia ya kwamba Yesu Kristo yu hai milele. Tujalie, Bwana. Yasikie maombi yetu.

242 Hili ndilo kusudi letu la kuwa hapa, Bwana. Na Wewe unayajua makusudi moyoni mwetu. Na kwa hiyo tunaomba ya kwamba Wewe utayapokea, Baba, tunapoomba baraka hii katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

243 Sasa, kwa utulivu kabisa. Sasa, hatuna saa ya ukutani. Ni yupi kati yenu ndugu? Niliivunja saa yangu ya mkono. Basi ni saa ngapi? Niambieni tu. [Ndugu fulani anasema, “Dakika saba baada ya saa nne.”—Mh.] Loo, nimechelewa kuliko nyakati zote. Kesho ni Jumamosi. Samahani. Niliona wawili au watatu wakisimama, kuondoka, na mimi—mimi najua nilikuwa nimekaa muda mrefu kupita kiasi. Hiyo ilikuwa . . . Jamani, ninyi ni watu wazuri sana! Ninachukia tu kuwazia ya kwamba

itanibidi kuwaacha usiku wa leo. Hiyo ni kweli, moyoni mwangu. Mimi ni . . . Ikiwa mimi ni mnafiki, sijui hilo. Lakini nawapenda watu.

244 Wakati nilipokuwa maskini mvulana mdogo, nikilelewa, hakuna mtu aliyenijali. Hakuna mtu aliyenipenda. Nami nikajiunga na kanisa, nikawekwa wakfu, kanisa Baptisti la Kimishenari. Daima nilikuwa na wazo ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu. Nami kwa namna fulani nilikuwa mtu anayeleta aibu, tuseme, kule.

245 Dak. Davis alizoea kuniambia, "Billy, utaishia kuwa mtakatifu anayejibingirisha," na yote hayo.

246 Lakini, bado, niliamini; kama Mungu aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Nami nilininii tu . . . Imani yangu iliniongoza njia hiyo, maana nilikuwa nimeona Hilo nilipokuwa mvulana mdogo. Na wengi wenu mmekisoma kitabu changu, hadithi ya maisha yangu, na kadhalika. Naye Mungu, Mbingu, inajua ni kweli. Nami nilijua kulikuwa na kitu fulani kule. Ningeweza kuiona Hiyo, ile Nuru. Iliongea nami, na tangu nilipokuwa mtoto mdogo mvulana, nami nilijua ilikuwa ni kweli.

Naye aliniambia, kasema, "Loo, uliota tu ndoto."

247 Nikasema, "Kama hivyo ndivyo ilivyo, nitaisalimisha tu kadi yangu ya ushirika."

248 Akasema, "Loo, usiwazie namna hiyo. Lakini," kasema, "utalishinda, Billy."

249 Lakini sijafanya hivyo, bado, na natumaini kamwe sitafanya hivyo. Hii ndiyo. Naye Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "*Hili* ni Lile." Kama *hii* siyo Ile, acheni tu niiweke hii mpaka Ile itakapokuja basi, kwa sababu naipenda *hii*. Nami naomba ya kwamba Mungu atamfanya kila mtu kujisikia hivyo.

250 Basi, enyi marafiki, ninawaambia yaliyo Kweli. Kufikia umbali huu . . . Hii hapa Biblia hii. Kamwe sijaifunga, bado. Kwa hiyo nisaidie, huku Biblia hii ikiwa moyoni mwangu, kwamba ninawaambia Kweli tupu.

251 Nami ninaamini ya kwamba ni Yesu Kristo, katika umbo la Roho Mtakatifu, mnaona, Mungu Roho Mtakatifu akishuka katika Jina la Yesu Kristo, kuthibitisha kwamba tuko katika siku za mwisho; na Roho Wake yuko duniani, miongoni mwa watu Wake. Nayo ile Nuru kule juu, ninaamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba hiyo ndiyo Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani. Ninaamini Hiyo ilikuwa Ndiyo ile ile iliyokuwa juu ya Yesu Kristo, ile ile wakati Yeye alipoondoka. Na Hiyo ni ile ile iliyoyapofusha macho ya Sauli, akienda zake Dameski, wakati aliposema kwa sauti kuu "Bwana, U Nani Wewe?" Naye akasema, "Mimi ni Yesu," Mnaona? Ninaamini ni kitu kile kile. Inafanya kazi zile zile.

252 Kwa hiyo, isingeweza kuwa ni mimi. Wazieni tu, mimi... Mimi sina hata elimu ya darasa la saba. Sijui lolote kuhusu, vema, elimu yo—yoyote, si zaidi ya angalau ile ya kuweza kusoma Biblia. Bali ninamjua Yeye.

253 Mtu fulani alisema, sio muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, huijui Biblia yako."

254 Nikasema, "Lakini ninamjua Mwandishi, ni—ni...vizuri sana. Na mimi...Yeye ata—Yeye atanijalia kukijua Kitabu Chake, kadiri Yeye anavyopenda kukifunua Hicho kwangu."

255 Na hapana wakati mmoja yule Malaika wa Bwana, aliyesimama pale, amewahi kuniambia hata wakati mmoja jambo lolote ila lililorudi moja kwa moja katika Biblia na kulithibitisha kwa Biblia. Kama aliwahi kuniambia chochote kilichokuwa ni kinyume cha Biblia, nisingekiamini. Biblia hii ni kwanza. Namna yoyote ya Malaika, ama chochote kingine, ambacho kingeshuhudia chochote kinyume na Neno hili, usikisikilize; Sijali jinsi linavyoonekana halisi. *Hili* ni sahihi. Daima ni sahihi.

256 Joseph Smith aliona—aliona malaika. Sasa, si—sitilii shaka neno la mtu huyo, hata kidogo. Lakini jambo lilikuwa ni kwamba, lilikuwa ni kinyume na Neno. Mnaona? Mimi—mimi—mimi...Halina budi liwe ni Neno. Ninaamini mtu huyo alikuwa ni mtu mzuri, hakika, na mwaminifu. Lakini mimi...

257 Yule ambaye huzungumza hapa, hana budi...Haipaswi kuwa ni chochote dhidi ya Neno hili. Halina budi kuambatana na Neno.

258 Na kwa hiyo nisaidie, sina wakati wa kukaa hapa, kuwaambieni, na usiku baada ya usiku. Lakini mambo mnayoyaona yakifanywa, ninaweza kuyathibitisha kwa Maandiko. Kama wewe huzichukua kanda, unajua hilo, ya kwamba ni tena na tena, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Inaelekeza hasa kwenye mti huu wa Bibi-arusi, majira haya, Roho yeye yule kurudi tena, na tunda la Roho Mtakatifu kudhihirishwa, "kuirudisha Imani ya watoto kwa Imani ya Baba zao tena." Ni kitu kile kile hasa, kote kupitia Biblia, kimetabiriwa kuwapo hapa. Nasi hawa hapa. Mara baada ya ubatizo kushuka, na mambo kama hayo, kunapaswa kuweko na kurejeshwa kwenye siku za mwisho.

259 Pia, enyi watu, msiiahirishe, angalieni huku nje kabisa katika siku za usoni. Kwa kawaida hiyo hupita juu ya kichwa chenu, na nyinyi—nyinyi hulikosa. Iweni tayari. Kama ni Maandiko, yashikeni. Kama si Maandiko, achaneni nayo. Mnaona? Lakini, basi anisaidie, ni Maandiko. Mnaona, hivyo ndivyo Yeye alivyofanya katika siku zingine. Kama Yeye ni yule yule leo, atafanya lilo hilo.

260 Sasa, ninaamini Billy Paul alisambaza kadi za maombi. Sivyo? Uliwapa nini leo? Tumepitia karibu hizo zote. Aha?

B, moja hadi mia moja. Vema, hebu tuanze. Tulikuwa wapi? Tulikuwa kwenye ya kwanza na ya mwisho, ya hizo zingine, na kupitia hapo. Si hiyo ilikuwa ni kweli. Hebu tuanzie nyuma kwenye ya kwanza, usiku wa leo, ya B, B, kadi za maombi zilizo na B. Na hebu tuanzie, vema, hebu tuanze tu kutoka namba moja, maana tutawafikia wote, haidhuru. Vema.

261 Namba moja. Ni nani aliye na B, namba moja, inua mkono wako. Mama huyu? Njoo hapa sasa. Kama wewe . . . ni . . .

262 Ninamwona mama mmoja kwenye kiti cha magurudumu pale. Na kama yeye, wakati kadi yake itakapoitwa, kama anayo, kumbukeni, mleteni tu moja kwa moja jukwaani. Mnaona? Ni sawa.

263 B, namba moja. Namba mbili? Namba mbili? Ni nani aliye na B, namba mbili? Yake ni namba mbili? Sasa, sawa, hebu kidogo. Hebu kidogo, tutaiingiza mstarini, mara tutakapoiita. Vema. Namba mbili, ni nani aliye nayo? [Ndugu fulani anasema, "Papa hapa chini, Ndugu Branham."—Mh.] Vema. Samahani. Samahani. Yuko nyuma ya maikrofoni. Huku, mama. Namba mbili.

Namba tatu? Vema, mama.

264 Namba nne? Kadi ya maombi namba nne, ni nani aliye nayo? Namba nne. Labda uiseme . . . Vipi . . . ? Hiyo ni nini katika Kihispaniola? [Ndugu mmoja anasema, "Cuatro."—Mh.] Cuatro. Ninajua sikulitamka vizuri. Kuna njia moja tu mimi . . . Neno moja tu ninaloweza kusema katika Kihispaniola, "Oiga." Ninakumbuka viziwi walikuwa wakisema, "Oiga," nawe unasema, "Sì." Vema.

Namba nne. Tayari yuko ndani, nne.

265 Tano, kadi ya maombi namba tano? [Ndugu fulani anasema, "Nyuma."—Mh.] Huko nyuma kabisa. Vema, mama mmoja hapa nyuma.

266 Mvulana huyo huleta kadi hizi huku chini sasa, na kuzisambaza hizi. Yeye huzileta mbele ya kusanyiko, anazichanganya kabisa, naye anakupa tu kadi ya maombi. Haijalishi uko wapi ama wewe ni nani, unaipata. Ndipo mmoja huenda akapata namba moja, huyo mwingine kumi na tano. Huyo mwingine . . . Na halafu bado hawajui mahali tutakapoanza kuitia. Mnaona? Na kwa hiyo mimi huja tu hapa, na popote tunapoitia.

267 Hiyo ni tano, sita, saba. Sita, inua mkono wako ikiwa unayo, sita. Sawa. Saba, namba saba? Vema. Nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne. Kumi na nne?

268 Sasa, ngoja kidogo, nimeona wawili. Nimekosea. Ni mwanamume na mwanamke wakienda kwingine. Nilifikiri walikuwa wakiamka, kuja.

269 Hebu tuone, kumi na mbili. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Kumi na tano? Kumi na tano? Kumi na tano.

270 Vema, hebu—hebu tuanze na hawa, maana tutawafikia wote. Tutamfikia kila mmoja wao, Bwana akipenda, katika muda mfupi tu. Lakini hebu. . .Hebu tungoje tu kwa dakika chache mpaka tu—tunapoweza kujua kama tu—tunaweza kuzifikia au la. Vema, kila mtu anajisikia vizuri.

271 Sasa, ni wangapi hapa ndani wasio na kadi za maombi? Hebu tuone mikono yenu. Vema. Sasa iweni na kicho. Angalieni huku. Ombeni. Sasa, kumbukeni, huu ndio mkutano wetu wa mwisho. Sasa hebu tuwe na kicho kabisa. Angalieni huku.

272 Sasa, wakati wanapoandaa mstari huo wa maombi kule, hebu tuseme hivi. Hebu turudi nyuma miaka michache. Hebu tumwone Bwana Yesu wakati mmoja, baada ya kuivuka bahari. Alifika ufukoni asubuhi, kutoka kwenye merikebu, na Yeye alikuwa akipanda kwenda bara. Ndipo maskini mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutokwa na damu, yeye hakuwa na kadi ya maombi.

273 Tuseme, ninaamini sisi. . .Mtu fulani amezima taa. Hiyo ni kwa kusudi fulani, ama nini? Ama zinajizima zenyewe? Je! wao. . .? Hiyo ni ya sisi kuondoka? [Ndugu fulani anasema, "La. Kitu fulani kilitendeka hapa."—Mh.] Loo, baadhi, baadhi. . . Loo, zinarudi. Mtu fulani alifanya kosa, huko nje, na kuzima swichi. Vema.

274 Mwangalieni sasa Bwana wetu Yesu. Sasa, ni wangapi wanaelewa hili? Hatujaribu kusema kwamba sisi ni Bwana Yesu. Mtu yeyote anafahamu hilo. Vema. Sisi ni ndugu zenu. Mnaona? Sisi ni watumishi Wake. Lakini, ni karama tu, kujisalimisha mwenyewe.

275 Sasa angalieni hili. Hawa hapa watu ambao ni—ni—ni—ni wanatheolojia, watu waliofunzwa katika Neno. Sasa, ndugu zangu, wakati nyinyi nyote mnapoanza kuhubiri ujumbe, kama ukijaribu tu kuubuni, wewe mwenyewe, haufai kitu. Sivyo? Lakini unapovuviwa, wewe—wewe, Huo kwa njia fulani unashuka tu. Hujui utakalosema. Hiyo ni kweli? Huko ni kuhubiri kwa uvuvio, mnaona. Huyo ni Roho Mtakatifu. Sasa, mimi, mimi sina ufasaha wa kutosha kufanya hivyo, kwa njia hiyo. Mnaona?

276 Lakini, sasa, kile yangu ilicho, ni karama tu, kujua tu jinsi ya kufanya, kama vile, kuvuta wenzo, na kujiondoa tu njiani. Na wewe. . .ni kujisalimisha tu kabisa. Siwezi kulielezea. Hakuna mtu anayeweza kumweleza Mungu. Siwezi kuwaambia jinsi ambavyo hiyo. . .kile kinachotukia, na kile kinachoendelea. Ninajua tu ni karama ndogo. Nami nina njia tu ya kujiondoa njiani. Halafu basi, mara ghafla, ninaanza kuhisi kitu cha kigeni, kitamu, kinyenyekevu. Na, tazama, ninaiona hiyo Nuru

ikizungukazunguka. Ndipo ninajua yote ni sawa. Hiyo ndiyo sababu mimi hungojea. Ndipo basi wakati mtu anapoanza kuzungumza . . .

277 Hiyo ndiyo sababu ninaye mtu fulani hapa juu, zaidi sana kama chambo, mnaona, kumtenganisha mtu mmoja, kusudi niweze kuzungumza nao. Ndipo basi Roho Mtakatifu anapoanza kutenda kazi juu ya mtu huyu, basi inaanza kulishika kusanyiko. Na ndipo kusanyiko linaanza ku—kushangaa, halafu wanaanza kupata imani. Ndipo, yeyote aliye na imani, basi unaanza tu kuihisi *hapa, pale*, kila mahali basi. Mnaona? Halafu tu . . . Hapo ni, inaithibitisha tu.

278 Sasa, kumbukeni, ni kitu kigumu sana, cha kuangamiza. Yesu angehubiri siku nzima; halikumsumbua. Bali wakati maskini mwanamke yule alipoligusa vazi Lake, kisha akaenda akaketi chini, iliondoa nguvu kutoka Kwake. Hiyo ni kweli? Vema, mtu yeyote anajua nguvu ni uweza. Vema, kama ingefanya hivyo kwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira, itatufanyia nini sisi kama wenye dhambi waliookolewa kwa neema Yake? Mnaona? Mnaona?

279 Kuhubiri, unaweza kufanya hivyo usiku kucha, hakutakusumbua. Lakini hebu ono moja tu litukie, unaona, ni kitu fulani, na ni katika ulimwengu mwingine. Unawaona watu labda walipokuwa watoto wachanga, ama kitu fulani. Nawe huna budi kuzungumza upesi; kwa sababu, unajua umesimama hapa, bali hata hivyo uko mahali pengine, huko nyuma kabisa mahali pengine, ukizungumza. Ndipo basi unapotoka kwenye hilo, hujui uliyosema mpaka uyasikilize kwenye kanda. Mnaona? Na si binadamu. Sio mtu. Hivyo tu. Ni Mungu. Daima ni sahihi. Na Yeye aliahidi hayo. Mnaona? "Kuyatambua mawazo yao," Biblia ilisema hivyo ndivyo Yeye alivyofanya. Iite chochote utakacho, lakini Biblia ilisema, "Yesu aliyatambua mawazo yao."

280 Sasa, ninawatakeni muamini. Sasa, kwanza, ninawatakeni muone jambo hilo, mnaona, sasa, kama uponyaji. Tunajua Roho Mtakatifu yupo hapa. Nami ninaamini katika kuwekea mikono.

281 Mtu fulani, loo, alinirukia, kidogo kwa fujo, kuhusu hilo, asubuhi ya leo. Kasema, "Hakuna kitu kama watu kuwekeana mikono mmoja kwa mwingine. Halipaswi kutendwa."

282 Nikasema, "Wewe hujaisoma tu Biblia, ndugu. Hivyo tu." Nikasema, "Agizo la mwisho, lililoshuka kutoka midomoni mwa Yesu Kristo, lilikuwa, 'Wekeni mikoni juu ya wagonjwa, nao watapata afya,'" Maneno ya mwisho Yeye aliyosema, wakati alipoondoka duniani.

283 Agizo Lake la kwanza, alilowapa wanafunzi Wake, lilikuwa, "Waponyeni wagonjwa, muwatakase wenye ukoma, muwafufue wafu, muwatoe pepo," lile kundi la kwanza alilolituma nje, Mathayo 10.

284 Nalo kundi la mwisho alilolituma, "Ishara hizi zitafuatana na hao, amini. Watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; watakunywa vitu vya kufisha. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hayo ndiyo Maneno ya mwisho Yeye aliyosema, na akapokelewa juu Utukufuni. Hakika. Hilo ndilo agizo kuu. Linachofanya, sijui mimi. Ni kutekeleza tu yale Yeye aliyosema tufanye.

285 Lakini hapa, wote, nadhani, asilimia tisini yenu, ni waaminio, ama zaidi. Nyinyi ni waaminio, nanyi mna haki sawa tu ya kuweka mikono juu ya wagonjwa kama nilivyo nayo mimi, ama waliyo nayo wachungaji wenu, kila mtu. "Wekeni mikono," waaminio, "ishara hizi zitafuata." Sio "wahudumu," bali kila mtu aaminiye. Mnayo haki, kila mtu.

286 Kama nilivyosema, hakuna watu wakuu, na watu watakatifu. Hakuna. Sisi, yeyote wetu, si mtakatifu. Tunaye Roho Mtakatifu ndani yetu, bali sisi si watakatifu. Ni, Yeye Ndiye aliye mtakatifu. Mnaona? Ni utakatifu Wake; sio wangu, sio wako. Wake!

287 Lakini, hapa, hebu na tufunge tu nia zenu kwa kila kitu sasa, kwa dakika kumi na tano zijazo. Na sasa, watu hawa wameketi hapa, wakiangalia kote.

288 Huyu hapa mwanamke amesimama mbele zangu. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Kadiri. . .Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine, mama? Mlimsikia, kile alichosema? Yeye alishakuwa katika mikutano yangu, mara kadha, bali hata hakupata nafasi ya kusema, "U hali gani?" kwangu. Mnaona? Hivyo basi, simjui mwanamke huyu. Amesimama hapo. Yupo hapa kwa sababu fulani. Sasa, hebu tu—tuwazie tu sasa. Tuchukue Yohana Mtakatifu, mlango wa 4, wakati Yesu alipokutana na mwanamke fulani.

289 Sasa, kumbukeni, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi pia mtazifanya."

290 Sasa, huyu hapa mwanamke na mwanamume, wakikutana kwa mara ya kwanza maishani. Sasa, hiyo ni kweli. Sisi hapa. Hii hapa Biblia ya Mungu. Huyo hapo mwanamke amesimama. Mimi huyu hapa nimesimama. Kamwe simjui, hata sijamwona mwanamke huyu maishani mwangu, ninajua. Hayo tu ndiyo nijuayo, ni, yeye amesimama hapo. Leo alikuwa hapa nje mahali fulani, na mtu fulani akampa kadi ya maombi, ndipo namba yake ikaitwa, naye huyu hapa amesimama. Hivyo tu.

291 Kunao wengi huko nje. Jana usiku tuliwachukua tu wale ambao hawakuwa na kadi za maombi. Ni wangapi waliokuwa hapa kuona jambo hilo? Mnaona, kadi ya maombi haina uhusiano wowote nalo. Mnaona? Ni imani yako ndiyo inayohusika.

292 Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, unaweza kuwaponya wagonjwa?" Hapana mtu duniani anayeweza kuwaponya

wagonjwa. Wameponywa tayari. Unapaswa tu kuwafanya wauone, wauamini.

293 Sasa, laiti Yesu Kristo angalijitokeza jukwaani na kutenda kazi kupitia kwangu na kwa mwanamke huyo! Sasa, kama ikitenda kazi kupitia kwangu na si kwake, haitafanya kazi. Haina budi kuwa ni sote wawili, pamoja. Mnaona?

294 Ni kama wewe. Kama una imani, unaiamini, basi, unaona, itatenda kazi kati yetu. Unaona? Ni imani yako na imani yangu. Nililiamini. Kama utaliamini tu pamoja nami, basi tutaona Maneno na ahadi za Kristo zikitimizwa.

295 Sasa, kama mtu yeyote anaamini ni makosa, nawe unaamini unaweza kufanya jambo lile lile, ninakualika jukwaani. Mnaona? Kwa hiyo, basi, usiseme chochote juu yake.

296 Sasa, njoo hapa, mama, simama tu hapa. Sasa, ninataka kukutoa nje, kwa sababu kuna imani kubwa sana. Nami ninataka kuzungumza nawe tu kwa dakika moja, kama Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke. Sasa, bila kukujua, sijawahi kukuona maishani mwangu, nawe ni mgeni kabisa kwangu. Sasa, kama Bwana Yesu atafanya tu jambo fulani hapa, kama alivyofanya wakati Yeye alipokuwa katika Biblia, siku ya Biblia, lingetufanya tujisikie tuna furaha, na—na tungeweza kwenda nyumbani?

297 Kama wale ambao, siku moja, Yeye alikuwa kwenye... Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Yeye alikuwa kwenye...Baadhi ya wanafunzi walikuwa njiani kwenda Emau. Unakumbuka hilo, ndugu? Njiani kwenda Emau, na—nao wakakutana na Bwana Yesu na kusemezana naye, siku nzima, nao hawakumtambua. Lakini wakati alipowaingiza ndani, usiku huo, na kuifunga milango, Yeye alifanya jambo fulani jinsi hasa alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, nao wakajua huyo alikuwa ni Yeye. Ni wangapi wanakumbuka hadithi hiyo? Hakika. Walijua ilikuwa, maana hakuna mtu mwingine aliyelifanya hivyo. Ndipo macho yao yakafumbuliwa, ndipo Yeye akatoweka kutoka kwao.

298 Sasa, Yeye yu hai usiku wa leo. Sasa, kama Yeye yu hai, basi atafanya vile vile leo kama alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, inathibitisha kwamba Yeye amefufuka. Hiyo ni kweli?

299 Sasa, Yeye hana mikono yoyote usiku wa leo ila mikono yangu na mikono yako. Ana macho katika yangu na yako. Hayo ndiyo Yeye anayotumia. Yeye ni Mzabibu. Sisi ni matawi. Hiyo ni kweli ndugu zangu? Nao Mzabibu hauzai tunda. Tawi huzaa tunda, likitiwa nguvu na Mzabibu. Hiyo ni kweli? Na kama tawi lile la kwanza lililotoka kwenye ule Mzabibu wa Kipentekoste, liliandika kitabu cha Matendo, kama mti huo ukizaa tawi lingine, litaandika kitabu kingine cha Matendo. Maana, ha—halitazaa mboga, kisha tikiti maji, halafu komamanga. Litazaa

tunda lile lile, kila wakati, maana ni Uhai ule ule ukipitia kwenye Mzabibu huo. Sasa mnaelewa?

300 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, wa Biblia hii, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa heshima na utukufu wa Mungu.

301 Sasa, kama wewe ni mkosoaji, usikae zaidi. Ni wakati wako wa kuondoka, maana, kumbuka, pepo waovu hutoka kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Na wengi hapa, ambao wamekuwako mikutanoni, wanajua kile kilichotukia. Kama wewe ni . . . Kaa tu kimya. Kama sivyo ulivyo; kama chochote kikitukia, nitawajibika.

302 Sasa, mama, sasa jambo fulani limetukia. Ni Uwepo Wake. Sasa, kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani ambalo umefanya, jambo fulani unalotaka kufanya, jambo fulani ambalo umefanya ama hujafanya, ama unalopaswa kufanya, ama jambo fulani kukuhusu wewe, utajua.

303 Kama tu vile alivyomwambia Simoni, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona.” Alimwambia jina lake. Akaamini. Yule mwanamke, Yeye alimwambia, “Una u— ugonjwa wa kutokwa na damu.” Kukakoma. Na Yeye akafanya ninii . . . ama kama ninii . . . Vema, kitu ambacho angemwambia mtu fulani, kwamba walikuwa na shida fulani, kama vile, yule mwanamke aliyekuwa na waume watano.

304 Kitu fulani, kitu tu kama hicho, mnajua ingekuwa ni Yesu Kristo. Unaliamini? [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Ingebidi itokane na nguvu za kimbinguni. [“Hakika. Najua hilo.”] Wewe, wewe unajua hilo. [“Ninajua hilo.”] Vema.

305 Sasa, sasa, kama mtu yeyote anaweza kuona, ile Nuru imesimama kati yangu na mwanamke huyu. Yeye anaihisi tu vile vile. Simjui mwanamke huyu. Lakini hebu mwulizeni tu jambo hili. Sikilizeni hili. Sasa hivi, kitu kama hisi tamu sana imekuja. Kama hiyo ni kweli, simama. Mnaona? Imemzunguka tu kote. Hivi hamwezi kuiona Hiyo? Ni upeo mwingine. Mnaona? Ninaiangalia Hiyo moja kwa moja. Sasa, ninapokuangalia, wewe ni mwaminio. Na una—unaugua. Naam. Moja ya shida zako kuu, ni, kwamba, wewe, wewe una wasiwasi sana. Na kupitia kwa wasiwasi huu, kumekufanya kuwa na shi—shinikizo kuu la damu. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Naam.

306 Mnaamini sasa? Sasa, kuona tu sasa, kwamba hai—haininii tu . . . Mnaona, ninaweza tu kumchukua mwanamke huyo mmoja na kusimama hapa, niendelee tu kuzungumza juu yake. Lakini, mnaona, wapo wengine wanaongojea mstarini. Mnaona? Wengine inabidi waje. Kwa hiyo, mnaona, yote haitakuwa juu ya mtu mmoja. Huna budi kumchukua mtu mwingine.

307 Lakini, sasa, mnge—mngetaka kuona kama Roho Mtakatifu angemwambia jambo jingine? Je! mngetaka? Inueni tu mikono yenu na kusema, “Ingenisaidia sana.”

308 Ingekusaidia? Vema. Hebu tuone. Sijui alichokwambia. Jambo pekee nijualo, itakuwa kwenye kanda. Sasa, hebu kidogo tu.

309 Niangalie tu na uamini. Kama vile tu Petro na Yohana walivyosema, “Tuangalie,” kwamba, kwa maneno mengine, “tupe usikivu wako.” Mnaona? “Basi Yeye alipoona walikuwa na imani.” Nami naona kwamba una imani.

310 Basi sasa, naam, ninaona ni kitu fulani kilichozunguka mkono wako. Loo, ni shinikizo kuu la damu. Daktari aliuzungushia mkono wako kitu fulani. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. A-ha. Na kusema, “Una shinikizo kuu la damu.” Na kuna jambo lingine. Loo, ninawaona. Wanaenda kutayarisha kitu fulani, kufanya, loo, ni upasuaji. Unajiandaa kwa ajili ya upasuaji. Na huo unahusu shida ya wanawake. Na hiyo inapaswa kuwa katika siku kadhaa zijazo kuanzia sasa. Hiyo ni kweli. [Dada huyo anasema, “Juma hili lijalo.”—Mh.] Hiyo ni kweli.

311 Sasa, mnaona ninalomaanisha? Mnaona? Kuendelea tu kumwambia, kuendelea kuzungumza naye, mengi yanaendelea. Mnaona ninalomaanisha? Mnaona?

312 Sasa, sio mimi. Mwulizeni mwanamke huyu kama ni kweli ama si kweli. Mwulizeni, mtu yeyote anayemfahamu. Mnaona?

313 Angalia huku tena. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Lingekusaidia? [“Ninajua Yeye anaweza.”] Bibi Dorns, unaweza kwenda nyumbani sasa na kuamini kwa moyo wako wote. Naam. Mnaona?

314 Mnamwamini Yesu Kristo sasa? Labda tuinue tu mikono yetu na kumwabudu Yeye basi. Yeye ni Mungu.

315 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili. Tunaomba sasa, ya kwamba Wewe utawaacha watu waone, kwamba tunaweza kuwa na ushuhuda, kwamba, Yesu yeye yule. Tunaweza kushuhudia asubuhi, ya kwamba, tulimwona Yeye. Yeye alikuwa hapa pamoja nasi usiku wa leo, katika umbo la Roho Mtakatifu. Tunakupenda Wewe, Bwana Yesu. Wafanye watu wote waone na kuamini. Tunaomba, Bwana, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, iweni tu wenye kuheshimika, wenye kicho, na heshima.

316 Sasa, sasa, mama huyu anayesimama hapa. Sasa, hivi sisi . . . Tunajua . . . hatufahamiani, nadhani, sivyo, mama, huyu mama aliyesimama mbele zangu? Hunifahamu. Hunijui. Sikujui. [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Lakini hajawahi kuniona maishani mwake. Vema. Sasa, hivi . . .

317 Mngali mnaamini, kila mtu? Iweni tu na kicho. Iweni tu na kicho kabisa. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Amina.

318 Nimeona jambo fulani likitukia. Nitangojea tu kwa dakika moja. Vema. Sasa angalia huku, kidogo tu, dada, wewe unayesimama hapa jukwaani. Kama sikujui mimi, bali Mungu anakujua, kama Yeye ataniruhusu kujua kitu fulani kukuhusu, ambacho—ambacho unajua. Kama sijui chochote kukuhusu, wewe ni mgeni tu kwangu. Bali kama Yeye atanifunulia jambo fulani, ambalo unajua kama ni la kweli ama sivyo, unaweza kushuhudia hilo, kama ni sahihi ama si sahihi.

319 Lakini, wewe ni, moja ya shida zako kuu, na shida yako kubwa zaidi, hiyo ni, ugonjwa wa wasiwasi. Unasumbuka, ambalo limekupa ugonjwa wa tumbo. Una ugonjwa wa tumbo na hali ya wasiwasi. Na ugonjwa huo wa wasiwasi hukupa ugonjwa wa tumbo, ambao husababisha mchachuko katika—katika sehemu ya chini ya tumbo. Ni kidonda cha mmeng'enyo kwenye sehemu ya chini ya tumbo. Shahamu na kadhalika hukufanya uteuke vitu. Na halafu ninakuona ukiondokea vyakula vingi mezani. Hiyo ni hakika.

320 Nawe umekuwa na mshtuko mkubwa ambao ndio kwanza ukujie. Umekuwa na msiba. Ni mauti. Ni mume wako, ambaye ndio kwanza aage. Limekutia wasiwasi. Hiyo ni kweli. Sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ninaamini utakuwa mzima sasa. Nenda, ukale chakula chako cha jioni. Yesu Kristo amekuponya.

321 Mnaamini? Iweni tu na imani kwa Mungu. Hivyo tu. Mnaona?

322 Sasa, mama huyu hapa, waweza kuangalia huku kwa dakika moja? Hatufahamiani. Hatufahamiani, bali Yesu Kristo anatujua sote wawili. Vema, sasa, kama Bwana Yesu atafunua jambo fulani kama ambavyo amefunua, kumwambia yule mwanamke, "Una waume watano," na wewe ni—wewe ni . . . ama, "Una kivimbe, kidonda, kansa; una matatizo ya kinyumbani," ama chochote kile, unajua ingebidi itoke kwa Mungu, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unaona, Yeye alimwambia tu mwanamke huyo jambo moja, nao mji mzima ukatubu.

323 Naye Huyu hapa, akifanya mengi zaidi sasa, kwa kuwa Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi nanyi pia mtazifanya, na nyingi kuliko hizi mtafanya." Ninajua King James inasema "kubwa zaidi," bali Emphatic Diaglott inasema "nyingi zaidi." Usingeweza kufanya kubwa zaidi; Yeye alikomesha maumbile, akawafufua wafu. Ungeweza tu kufanya nyingi zaidi ya hayo, unaona, wingi badala ya ubora.

324 Unaugua, pia, ugonjwa wa wasiwasi. Una shida ya wanawake, ambayo ni ugonjwa wa kike. Pia una ugonjwa wa tumbo unaokusumbua. Hiyo ni kweli. Unaamini Yeye anaweza kukuponya? Unaamini atakuponya? Una mtu fulani moyoni mwako, sivyo? Mume wako. Hayupo hapa. Unaamini ninaweza kukwambia nini. Kama Yesu atafunua shida ya mume

wako, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Yeye ana wasiwasi kabisa, na umemfanya kushikwa na ugonjwa wa tezi dume. Hiyo ni kweli. Sivyo? Kuwa na imani. Usitie shaka. Amini tu, kwa moyo wako wote.

325 Hapa, hebu kidogo. Kitu fulani kinaendelea. Naam. Hiki hapa. Ni mama yako. Huyo ndiye, aliyeketi pale pale nyuma, mwishoni mwa kiti. Ana ugonjwa wa kutetemeka. Nawe unamwombea. Hiyo si ni kweli? Bibi Harris, hilo ndilo jina lako. Amini kwa moyo wako wote, kisha urudi. Weka mikono yako juu ya mume wako, mama yako, na wapate afya, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

326 Iweni na imani kwa Mungu. Mnamwamini Mungu? Sasa, nafikiri inatupasa tu kumwabudu Yeye. Sivyo? Hebu tumsifu tu Yeye, tuseme, "Asante, Bwana mpendwa."

327 Baba wa Mbinguni, jinsi tunavyokushukuru Wewe, kukusifu Wewe! Jina takatifu la Bwana Yesu Kristo na libarikiwe. Tunakupa utukufu, heshima, shukrani, na sifa, na nguvu, katika Jina la Yesu. Amina.

328 Iweni na imani. Msitie shaka. Amininі tu yale Mungu amesema ni Kweli. Hivyo tu ndivyo mnavyopaswa kufanya. Sasa iweni na kicho kabisa na mwangalie upande huu.

329 Sasa, huyu hapa mwanamume. Hatufahamiani, bali Yesu Kristo anatujua sote wawili. Unamwamini? Unaniamini kama mtumishi Wake? Utaamini.

330 Sasa, wakati Yesu alipokutana na mwanamume fulani, ilikuwa, ambaye tunamwona akimfanyia mwujiza, alikuwa ni Simoni. Sivyo? Huyo alikuwa ndiye mwanaume wa kwanza aliyekutana naye. Vema. Alimwambia Simoni jina lake lilikuwa ni nani.

331 Sasa, Bwana na anisaidie kujua shida yako, kwamba ndiyo. Naam, ninaiona sasa. Ni ugonjwa wa matumbo: utumbo mpana. Ni utumbo mpana uliovimba. Hutoki hapa, pia. Unatoka Magharibi, upande *huu*. Unatoka California.

332 Kuna mtu aliye pamoja nawe. Anayo kadi ya maombi, akaombewe, usiku wa leo. Ameketi huko nje sasa. Yeye ni rafiki yako. Naye ana ugonjwa wa wasiwasi, kama kurukwa na akili. Unaamini yeye atapona? [Huyo ndugu anasema, "Haleluya!"—Mh.] Nami pia. Unaamini sasa ya kwamba Yesu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Bw. Hamby. Basi, rudi, weka mikono yako juu ya rafiki yako. Na uamini kwa moyo wako wote, na nyote wawili mnaweza kurudi na kupata afya, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

333 Mnaamini? Sasa ombeni. Imenidhoofisha kabisa. Na inaanza sasa hivi, mnaona. Ombeni. Nasi tutaanza tu kuwaombea wagonjwa sasa.

334 U hali gani? Unazungumza Kiingereza? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, ninazungumza.”—Mh.] Unazungumza. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? [“Ninaamini.”] Hivyo ndivyo Malaika alivyoniambia, kasema, “Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini.” Sio kuniamini mimi kuwa ni Yeye, bali kuamini Yeye alinituma. Ni kwa ajili ya mvulana wako mdogo. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? [“Naam.”] Utaamini? [“Naam, nitaamini.”] Yeye ana wasiwasi. Umetokana na tishio. Mbwa alimtisha. Hiyo ni kweli. Atakuwa mzima. Mrudishe. Amini kwa moyo wako wote, atakuwa mzima. Ni mshtuko. Nitaweka mikono yangu juu yako, katika Jina la Yesu. Usiogope. Usiogope, naye atapata ushindi dhidi yake, na kuwa mzima. Unaona? Kuwa na shukrani.

335 Mnaamini kwa moyo wenu wote? Amina. “Kama unaweza kuamini.”

336 Mama huyu anayeketi hapa, akizungumza na yule mwingine pale, akiwa na ugonjwa huo wa mapindi. Muda mfupi uliopita, ambapo kitu fulani kilikufanyikia, hicho ni mapindi yako yaliponywa. Amina. Wewe amini, kisha uende nyumbani sasa na uwe mzima. A-ha.

337 Mnaamini? Huko nje katika kusanyiko, mnaamini?

338 Unawaza nini, huku mkono wako umeinuliwa, unayeketi huko nje? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Basi hiyo ngiri haitakusumbua tena. Mke wako ni mgonjwa sana. Madaktari hata hawajui shida yao. Weka tu mkono wako juu yake, amini kwa moyo wako wote. Yeye anajua shida yake. Atapata afya, kama utaamini.

339 Unaamini Mungu aliuponya ugonjwa wako wa moyo, unayesimama hapo? Basi rudi nyumbani, ukapate afya.

Sasa, kama huyu siye Yesu Kristo miongoni mwetu!

340 Unawazia nini juu yake, maskini mama unayeketi hapo ukiniangalia moja kwa moja, hapo kwenye safu ya pili? Ana ugonjwa wa kifua. Unaamini Yesu Kristo anakuponya? Simama kwa miguu yako na uukubali basi. Amina.

Iweni na imani kwa Mungu. Msilitilie shaka.

341 Mama yule pale, nilimwangalia, na kidogo nikamhurumia, fulana nyekundu, aliyeketi. Una ugonjwa wa mapindi. Unaamini Bwana Yesu anakuponya? Naam. Simama kwa miguu yako na kuukubali, na upate afya. Amina. Hiyo ndiyo njia ya kuifanya. A-ha.

342 Unafikiria nini juu yake, unayeketi hapo, ndugu? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako? Mzio wako umekwisha. Yesu Kristo anauponya. Haleluya!

343 Unaliamini, kwa moyo wako wote? Amina.

344 Ati? Tulisimama wapi, kadi ya kumi na tano? Ilikuwa hiyo, kadi ya maombi kumi na tano? Ni wangapi wengine walio na kadi za maombi hapa ndani? Hebu tuachane na hizi kadi za maombi. Fanyeni foleni hapa chini upande huu.

345 Hebu niwaonyeshe. Hebu niwaonyeshe kwamba uponyaji si mali ya mtu mmoja tu. Hebu niwaonyeshe kile Mungu anachoweza kufanya kupitia watumishi Wake wanyenyekevu hapa. Njoni hapa, ndugu. Sijui kama ninyi ndugu mwaweza kuja papa hapa chini, papa hapa pamoja nami. Tembeeni, shukeni moja kwa moja mtoke jukwaani, mje papa hapa chini kwa dakika moja. Naam. Vema. Tunaenda kufanya hivyo. Tutawaombea papa hapa. Ninawataka watu waone jambo hilo, kwamba Mungu huwatumia watumishi Wake. Njoni. Njoni. Nyinyi, nyinyi wahudumu, njoni papa hapa chini. Ninashuka hapa chini pamoja nanyi. Mnaona? Nitawaonyesha ya kwamba Mungu huwaponywa wagonjwa kupitia wachungaji wenu. [Ndugu fulani anasema, "Ati chini, tuondoke jukwaani?"—Mh.] Haijalishi, vyovyote vile mnavyotaka kufanya. Amina. Hilo ni sawa.

346 Nyinyi watu wote mlio na kadi zenu za maombi, njoni hapa juu. Kamwe usilitilie shaka. Wewe amini. Unaamini kwa moyo wako wote sasa?

347 Sasa, wachungaji, baadhi yenu huko chini, ninataka kila mmoja wenu. Wakati nikiomba, ninawataka ninyi nyote, baadhi yenu mshuke mwende kule, na uhakikishe kwamba mkono wako unamgusa kila mtu kwenye mstari huo. Mnaona? Siwezi kumfikia kila mmoja wao, bali mnaweza. Ndivyo hivyo. Shukeni mwende kule, mwende moja kwa moja miongoni mwao.

348 Ninyi watu wote huko nje, aminini sasa. Tutawafikieni kwa dakika moja. Aminini pamoja nasi sasa.

349 Kila mmoja wenu nyote hapa, kumbukeni, Yesu Kristo anakujua. Anajua hasa kile unachofikiria. Mnajua hilo. Hakuna mmoja wenu ila ambaye Yeye angekwambia sasa hivi. Mnaona hilo. Basi Yeye yupo hapa. Ni Yeye. Sio mimi. Mimi ni ndugu yenu tu.

350 Sasa aminini, wakati nikiomba. Ninaenda kuwaombea, pamoja na wachungaji hawa.

351 Mnaona, sitaki kuondoka mjini, watu wanafikiri, "Vema, yule mwinjilisti alikuwa humu ndani. Alifanya *hili*." Ninawatakeni mjue kwamba mchungaji wenu ana mamlaka yayo hayo. Huenda asione maono; hayo labda huja mmoja katika kizazi kimoja. Lakini—lakini yeye ana mamlaka yayo hayo kutoka kwa Mungu, kuweka mikono yake juu yenu. Ni vile vile hasa.

352 Sasa hebu na tuombe sote. Endelea kuinamisha kichwa chako sasa. Na kila mmoja wenu, utakapohisi mikono ya mchungaji huyo imekugusa, kumbuka tu, iangushe kadi yako ya

maombi, inua mikono yako, na umshukuru Mungu kwa ajili ya uponyaji wako, kisha urudi pale na uone kitakachotukia.

353 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika hapa sasa katikati ya watu hawa, katika Uwepo wa Mwenyezi Mungu, Ee Yehova mkuu wa Milele, Yule aliyemleta Yesu Kristo, Mwana Wako. Ninaomba sasa, wakati wahudumu hawa, mikono ya Mungu. Na ninapoweka mikono yangu juu ya dada yetu hapa, ninaomba ya kwamba Wewe utakutana nao, Bwana, kila mmoja. Jalia nguvu za Yesu Kristo zishuke juu ya kusanyiko hili sasa hivi, wakati wachungaji hawa wakiwagusa watu hawa. Pia jalia kila mmoja wao aponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

354 Shetani, umepoteza ushindi. Yesu Kristo yupo, kuzitia upako leso hizi, kuwaponya wagonjwa, kufanya kazi aliyoahidi kufanya. Na sisi, kama watumishi Wake, tunakusahi, kwa imani yetu wenyewe katika kufufuka Kwake, katika Uwepo Wake sasa, baada ya miaka elfu mbili, akitenda kazi kiroho kupitia Kanisa Lake. Toka ndani ya watu hawa. Katika Jina la Yesu Kristo, waachilie waende. Toka, kupitia Jina la Yesu Kristo.

355 Sasa, wakati wakiweka mikono juu ya wagonjwa, kama kuna mwenye dhambi, ama mtu anayetaka kuokoka, anayetaka kuja karibu na madhabahu sasa, basi, simama moja kwa moja na uje mbele sasa. Tupo hapa kuhudumu. Kama wafanyakazi wa kibinafsi wakija pamoja nao, wanaosimama na kuja.

356 Yeyote anayetaka kuja hapa juu kwa ajili ya maombi sasa, njoo moja kwa moja mbele. Kama una kadi ya maombi ama huna, umekaribishwa kuja papa hapa sasa, upate kuwekewa mikono. Njoo sasa, wakati tukingojea.

357 Kukiwako na mmoja wenu ambaye ni mhitaji, anayemhitaji Roho Mtakatifu, anayehitaji wokovu, anayehitaji uponyaji wa Kiungu, tupo hapa, kama wahudumu wa Kristo, kukutumikia katika wadhifa wa kuwekea mikono, na kukuona umejazwa na Roho.

358 Kila mtu ambaye angetaka kuwa na huyu Yesu ajuaye siri za moyo wako! Ninyi watu msiomjua, na mnaihisi maskini hisi hiyo ya kigeni moyoni mwako, najua wapo hapa. Roho Mtakaifu ananiambia hivyo. Njoni hapa juu sasa. Njoni hapa juu. Kama utasimama kutoka kitini mwako na uje huku, na kusema, "Bwana Yesu, naja kwa sababu ninakuhitaji Wewe, nami ninakuja kukupokea Wewe," Mungu atakujalia haja yako kama hutatilia shaka. Basi amini kwa moyo wako wote ya kwamba mambo unayoona sasa hivi ni kazi za Yesu Kristo! Kama wewe ni Mmethodisti, njoo. Kama wewe ni Mbaptisti, Mnazarayo, Mpilgrim Holiness, Mkatoliki wa Kirumi, Myahudi wa kiothodoksi, mwenye dhambi aliyevunda, kafiri; Sijali wewe ni nani. Tembea uje hapa juu, ukimwamini Mungu, na uone kinachofanyika sasa hivi. Njoo. Ninataka kuwaona mmekusanyika hapa.

359 Ninaamini, Roho Mtakatifu, kwenye wakati huu muhimu sana, majira haya makuu, ambapo hata tumepitiliza wakati, lakini, hata hivyo, ninaamini ya kwamba sasa hivi Mungu anaenda kutimiza haja yako kama tu ukiniamini. Mmemwona Yeye akichukua . . . Hakika ninawaambia Kweli.

Vema, dada, unaweza kushuka uende moja kwa moja pale, ukaponywe. Unaona?

360 Sasa, hakika mtaniamini. Kuna kila mmoja wenu hapa sasa ambaye ana haja ya Mungu. Njoo, simama, ama simama upande huu. Mahali fulani, simama tu kwa miguu yako, kuwa shahidi, useme, "Ninashuhudia, Bwana," na halafu kama kuna kasoro fulani. Simama mahali ulipo. Simama moja kwa moja kama u—kama una haja na Mungu. Hiyo ni sawa. Kama huwezi kusimama . . . Jambo ndilo hilo. "Nina haja na Wewe, Kristo."

361 Sasa, naomba mniamini. Je! mnaniamini? Mnaamini huyo ni Mungu anayenena nami? Kama mnaamini, inueni mikono yenu, kama mnaamini. Asanteni. Sasa, kwa sababu mnaamini . . . Kama nimewaambia Kweli, Mungu ni shahidi, nimewaambia Kweli. Mungu yupo hapa, shahidi, niliwaambia Kweli.

362 Sasa, ninawaambia Kweli sasa. Kama mtamtazamia Mungu, na kwa imani mseme, "Bwana Yesu." Kama wewe ni mwenye dhambi, sema, "Nakiri dhambi zangu." Kama unataka Roho Mtakatifu, sema, "Bwana, na—nahitaji baraka Zako, kunipitisha maishani. Ninamtaka Roho Mtakatifu." Ikiwa wewe ni mgonjwa, sema, "Ninahitaji uponyaji, Bwana, na sasa ninaukubali kutoka Kwako. Ninauamini." Kama utafanya hivyo, basi utaupokea.

363 Sasa hebu tuinue tu mikono yetu, kila mmoja kwa njia yako mwenyewe. Inabidi iwe ni maungamo yako. Nami ninaenda kuwaombea hapa. Sasa ninyi aminini, na mwombe. Ninaenda kukuombea, nawe ujiombee mwenyewe. Omba tu. Kiri makosa yako mwenyewe. Ungama udhaifu wako. Toa ahadi yako kwa Mungu kwamba wewe si dhaifu tena; una nguvu. Wewe si mwoga. Hutakuwa mgonjwa. Hutatumikia dhambi tena. Utamtumikia Mungu. Fanya maungamo yako na uamini. Ni nafsi yako. Ni jukumu lako. Hiyo ni kweli.

Mtu fulani aligusa moto. Hiyo ndiyo njia ya kuifanya. Amini tu hilo.

364 Bwana Yesu, hii saa kuu iko hapa, ule wakati mkuu, muhimu sana. Siku ya mwisho ya karamu iko hapa, wakati wa mwisho, nafasi ya mwisho. Watu hawa wana haja. Jalia Roho Mtakatifu ashuke, Bwana. Jalia watu wamwone Huyo, wamhisi Huyo, wajue kwamba huyo ni Mungu, Kristo katika maisha yao, akijaribu kuingia kwenye wakati huu, na kuwapa shauku kubwa zenye kilindi mno za moyo wao. Lijalie, Bwana. Jaza . . . wao kwa Roho Mtakatifu. Waponye wagonjwa. Jipatie utukufu kwa Jina Lako.

365 Sasa, Shetani, umeshindwa vita. Umeshindwa mkutanoni. Umepoteza ushindi. Ninadai ushindi, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya kila mtu hapa ndani. Toka mahali hapa, Shetani. Huwezi kuwashikilia zaidi. Ninawadai, tunu, kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo. Amina.

63-0607 Msiogope
Ramada Inn
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org